Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:31 PM Page A

# FALSAFA YA DINI

Kimeandikwa na:
**Sayyid Jawad Naqvi**

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:31 PM Page B

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**

**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 17 - 004 - 3**

Kimeandikwa na:

**Syed Jawad Naqvi**

Kimeandikwa na:

**Sayyid Jawad Naqvi**

Kimetarjumiwa na:
**Dk. Muhammad S. Kanju**

Kimehaririwa na:
**Alhaj Ramadhani S.K. Shemahimbo**

Kimepangwa katika Kompyuta na:
**Hajat Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Oktoba,2011
**Nakala: 1000**

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
**Alitrah Foundation**
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:31 PM Page C

# YALIYOMO

Utangulizi.. .......................................................................................2

Ni kipi kinatupasa kiwe ni mahusiano yetu na dini? ................................3

Tofauti kati ya Madhumuni na Manufaa ..................................................7

Madhumuni na Manufaa ya Dini ............................................................11

Falsafa ..................................................................................32

Maswali ..................................................................................36

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:31 PM Page D



بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَـٰنِ ٱلرَّحِيمِ **Yeye ndiye**

﴿ هُوَ ٱلَّذِى بَعَثَ فِى ٱلْأُمِّيِّـۧنَ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا۟ عَلَيْهِمْ ءَايَـٰتِهِۦ وَيُزَكِّيهِمْ
وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلْكِتَـٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا۟ مِن قَبْلُ لَفِى ضَلَـٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٢﴾ ﴾

**Aliyempeleka Mtume kwenye watu wasiojua kusoma, aliyetokana na wao, awasomee Aya zake, na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, japokuwa hapo kabla walikuwa katika upotofu uliodhahiri. (Qur'an 62:2).**

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:31 PM Page E



بسم الله الرحمن الرحيم

## NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, *Philosophy of Religion,* kilichoandikwa na Sayyid Jawad Naqvi. Sisi tumekiita *Falsafa ya Dini.*

Kitabu hiki huelezea kwa ujumla falsafa na hekima ya dini na jinsi ya kuifuata dini pamoja na changamoto zake. Mwandishi ameandika kitabu hiki kwa kuwalenga Waislamu wa Pakistan na India ili kuwaasa kwa ajili ya masaibu wanayoyapata mikononi mwa mabeberu. Lakini hali hii ipo pia katika nchi nyingine za Kiislamu, kama vile Iraq, Afghanistan, Palestina, na inanyemelea nchi nyingine za Kiislamu na kwa Waislamu popote wanapoishi ulimwenguni. Hivyo, ni jukumu la kila Mwislamu popote alipo kuchukua tahadhari na kuungana na Waislamu wote ulimwenguni kuukataa unyanyasaji huu unaofanyiwa Waislamu.

Waswahili wanasema: “Ukimwona mwenzako ananyolewa, wewe tia maji kichwa chako.” Lakini pia tunajifunza kutokana na makosa ya wenzetu. Leo hii ni Pakistan, kesho ni Kenya, na keshokutwa ni Tanzania. Hili ni somo la kuzingatiwa.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa utandawazi ambapo dunia imekuwa kama kijiji. Hakuna linalotokea upande mwingine wa dunia bila kuugusa upande mwingine.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, Dk. M. S. Kanju kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni changamoto kubwa kwa wasomaji wetu, hususan Waislamu ambao ni waathirika wakubwa kutokana na dhulma na unyanyasaji huu.

**Mchapishaji:**

**Al-Itrah Foundation**

# Dibaji

Dini ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuishi imekuwa muathiriwa wa misiba mingi matokeo yake ambayo yako wazi leo ambapo dini nyingi za uipotofu zilizotengenezwa na watu zipo miongoni mwetu. Sababu ya yote haya ni kukosekana kwa ukamilifu au uelewa wa madhumuni ya dini.

Mwamadamu ameibadilisha ili kukidhi malengo mbaimbali lakini mengi ya hayo hayako hata karibu na madhumuni ambayo kwamba yamekusudiwa katika dini kwa ajili ya mwanadamu.

Mtu lazima afanye juhdi ili kupata dini sahihi ambayo inaweza kukamilisha madhumuni ya maisha na kumpa wokovu na maisha mazuri katika dunia na Akhera. Lakini ili kufanya hivyo ni lazima katika hatua ya kwanza aelewe filosofia ya Dini. Ni nini kinachomaanishwa na Dini? Ni jukumu gani Dini inafanya katika maisha ya mwanadamu na ni malengo gani hayo ambayo Dini inataka mtu ayafikie? Haya ni baadhi ya maswali ambayo yanalengwa kushughulikiwa katika kitabu hiki kwa jina la "**Filosofia ya Dini**.

Utambuzi wa ujuzi wa Mwandishi Syed Jawad Naqvi katika nyanja ya filosofia ya Kiislamu ukiunganishwa na mtindo mzuri wa uwasilishaji wa habari changamani katika hali ya kimantiki na kueleweka humfanya kuwa mwandishi bora katika eneo hili atakalo. Tumefanya tarjuma ya mada hii katika Kiingereza (na sasa katika Kiswahili) kwa ajili ya wasomaji wa Kiingereza (na sasa kwa ajili ya wasomaji wa Kiswahili ili nao wapate manufaa kutokana na ujuzi na taarifa muhimu za kina ambazo anazo mwandishi huyu.

Kitabu hiki kimekusudiwa tu kupanua uoni wa mtu na hususan wale ambao wanaheshimu dini na wanajaribu kuwa wanadini lakini hawana ujuzi au utambuzi wa dini ya kweli kwa sababu bado hawajaifuatilia dini kwa mtazamo wa kifilosofia. Insha-Allah kitabu hiki kitawasaidia wasomaji kuanza safari ya kuitambua dini.

**Syed A .V Rizvi**

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:31 PM Page 1



Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:31 PM Page 2



# Utangulizi

Mada iliyoko kwenye mjadala ni Filosofia ya Dini, suala ambalo ni la muhimu sana lakini mara nyingi halizungumziwi au kuandikwa. Hii ndiyo sababu watu wanaweza kuuliza ni nini madhumuni ya kujadili Filosofia ya Dini?

Filosofia ya Dini haina maana ya filosofia ya kidini, kwa sababu filosofia yenyewe ni tawi la elimu, na kama ilivyo njia nyingine za elimu, ni muhimu kwamba tunajua kuhusu dini zetu pia.

Madhumuni yangu sio kujadili filosofia ya dini mahususi bali kupata mjadala wa msingi kuhusu dini. Kwa kawaida, kizazi cha sasa huuliza kwa nini wanapaswa kufuata njia ya dini. Ni haja ipi inayoridhiwa na dini? Wanahitaji jibu la swali hili na ni matatizo gani inayotatua? Kama ingekuwa hakuna dini, je, ingemuathiri mwanadamu kwa namna yoyote?

Kijana wa leo anaishi katika ulimwengu uliozungukwa na wafuasi wa Uislamu, wasio wafuasi wa upagani, wengi waliomzunguka ni Waislamu lakini katika jina tu na kuna wangine ambao ni waumini wa kwelikweli katika Uislamu na kuufuata pia. Akiangalia pembezoni mwake anaona kwamba, kimatendo kuna tofauti ndogo kati ya maisha ya muumini na asiye muumini, wote ni wanadamu, wote wanakula na kunywa.

Kinyume chake, anaona kwamba wasio waumini na maadui wa Uislamu wanaonekana wenye furaha zaidi na wenye ustawi zaidi kuliko waumini. Ni nini basi madhumuni ya dini, anashangaa. Anauliza, kuna haja gani. Kwa kawaida mahatibu na wahubiri huzungumzia tu misingi ya Uislamu. Kwa kweli, kuna elimu ndogo sana kuhusu dini inayopatikana kutoka kwenye Madrasa, hutuba kwenye mikusanyiko yetu na majilisi zetu za maombolezo.

Hapa neno Madrasa lina maana ya njia zetu za kwaida tulizozoea za kufundisha watoto wetu, ambazo husisitiza katika kusoma Qur'ani kanuni za msingi za ibada bila ya kutumia mantiki na hoja.

## Ni nini kinapaswa kuwa ni mahusiano yetu na dini?

Kwa nini nahitaji dini hii? Itakuwa na maana gani kwangu? Mpaka hapo maswali haya yatakapojibiwa, bongo na akili za wanadamu haziwezi kuridhika kikamilifu.

kuna sura nyingi tofauti za wafuasi wa Uislamu tunazoziona leo kama:

a. Kuna baadhi ambao kitendo chao tu cha kidini ni kusali mara moja kwa mwaka wakati wa Iddi.

b. Kuna wengine ambao mawasiliano yao tu na dini ni kwa zile siku kumi za wakati wa Muharram.

c. Kuna baadhi ambao hutumia muda wao tu kuhudhuria sala za Ijumaa tu.

d. Kuna wengine ambao husali sala zao za wajibu za kila siku bila kukosa.

e. Kuna wengine ambao, kwa nyongeza ya sala za wajibu, hujaribu na kutekeleza Uislamu katika maisha yao ya kila siku.

f. Kisha kuna wale ambao wmjitolea katika njia ya Uislamu na wanajishughulisha usiku na mchana katika njia ya Uislamu

Wakati mwingine, kwa kuwafundisha watu kanuni za misingi ya Uislamu, tunaamini kwamba amepata ujuzi wa kutosha kuhusu dini na ataendelea kuwa katika njia sahihi. Lakini haitokei hivyo. Kwa kujifundisha tu kuhusu dini, kwa hakika anakuwa haielewi dini kama anavyopaswa kuwa.

Kwa mfano, kuna watu wengi hujifundisha kuhusu Uislamu katika shule zetu za Kiislamu za kawaida (Madrasa) lakini kwa hakika hawautekelezi katika maisha yao ya kila dini. Wanajua kila kitu kuhusu dini, lakini hakuna dalili ya Uislamu katika maisha yao ya kila siku. Kuna watu wengi ambao wamejifundisha Uislamu na wakauelewa, lakini hata hivyo hatuoni dalili zozote za dini katika maisha yao ya kila siku. Nani anapaswa kutueleza kuhusu dini na utekelezaji wake wa kimatendo? Inawezekana kwamba hata baada ya kujua kuhusu dini, mtu anaweza kupotoka; anaweza kuifikiria dini kama kitu kisicho na umuhumu au lazima katika maisha yake.

Swali ambalo linalojitokeza sasa ni kwamba ni upi utakuwa uhusiano wetu na dini? Ni orodha ndefu. Kila mtu ana uhusiano maalimu na dini; anaiona kutokana na mtazamo wake binafsi. Nani atamuambia ni vipi uhasiano wake na dini unavyotakiwa kuwa?

Jibu kwa maswali yote haya ndicho kinachotakiwa kuwa uhusiano wetu na dini. Kwa nini dini ni muhimu kwa mwanadamu? Ni matatizo gani yanatatuliwa na dini? Je, maisha ya mwanadamu yatakuwa na tofauti yoyote bila dini? Je, kuna tofauti ya maisha kati ya kafiri na muumini?

Mjadala ambao kwamba unajibu maswali yote haya ni Filosofia ya Dini ambayo maana yake ni kuzungumza kuhusu Dini. Hii ina maana katika muktadha huu (Filosofia ya Dini) hatutazungumzia kuhusu itikadi za kiutendaji za dini kama vile ni Rakaa ngapi katika sala, au jinsi ya kufunga au kuhiji.

Hatutajadili kuhusu misingi ya Uislamu. Haya ni masuala yanayohusiana na dini yenyewe na hujitokeza yenye kuhusika tu wakati mtu anapoamua kwamba anahitaji dini. Imani ya kawaida ambayo imekuwepo kwa zama kadhaa; moja ambayo imekuwa ikitangazwa na wazazi wetu na watu wa makamo yao, halikadhalika na kuenezwa na Madrasa zetu, Misikiti na Hussainiyah (Kumbi za kufanyia hafla za dini) ni kwamba dini ni biashara

ya kukopesha. Ikimaanisha kwamba, unaifanya hapa na utapata malipo baada ya kifo chako.

Kuna faida kubwa zaidi katika aina hii ya biashara. Lakini hiyo inaweza isiwe hivyo kila siku. Mtu anayetoa mkopo atakuwa na wasiwasi kuhusu kulipwa deni lake. Atakuwa na wasiwasi kuhusu kitakachotokea kwenye mkopo wake kama mtu akifa. Kama unataka kununua kwa wingi kwa mkopo, mfanyabiashara yeyote atasita kukupa. Lakini kama ukijitolea kulipa nusu ya gharama kwa pesa tasilimu, basi anaweza akakubali. Lakini kama mtu mwingine yuko tayari kulipa gharama yote kwa pesa tasilimu, hatakukubalia wewe.

Kama una wanunuzi wawili na mmoja wao akajitolea kukulipa bei ya juu kwa bidhaa fulani lakini kwa mkopo, na yule mwingine akajitolea kukulipa nusu ya bei kwa pesa tasilimu kwa bidhaa hiyohiyo, basi kwa hakika hutamkubalia yule mtu wa kwanza. Ina maana utapendelea biashara ya pesa tasilimu kwa sababu hujui iwapo mtu yule atakulipa hapo baadae au la. Jinsi ambavyo tunahubiri dini huonesha kwamba dini ni mali lakini katika muundo wa mkopo tu. Watu wanaahidiwa kwamba kama wakifanya kazi kwa bidii, kusali mchana na usiku, kufunga na kukabiliana na shida katika ulimwengu huu, watapata malipo baada ya kufariki kwao wakati wa Kiyama (Siku ya Malipo). Hakuna ajuaye Kiyama kitatokea lini na wengi wana shaka iwapo kweli Kiyama kitatokea.

Wakati mwingine baadhi ya watu, kwa ajili ya masilahi ya binafsi, hugeuza nadhari ya watu kuelekea kwenye masuala yasiyo na umuhimu. Kama inavyotokea kwenye baadhi ya nchi ambazo serikali zao sio imara, wakati serikali hizi zinapokuwa legelege ili kuwapumbaza raia wanaandaa matukio ya baadhi ya michezo mikubwa maarufu katika nchi zao kama vile mpira wa miguu, kriketi Vile watu wanavyojishughulisha na kuangalia michezo kama hiyo kwenye TV, wanasiasa nao wanacheza ya kwao michezo (ya kisiasa). Wahubiri wa dini nao vilevile wanacheza mchezo huohuo. Huwashughuligha watu na wao kufurahia maisha ya anasa na

starehe. Huwaambia watu kuendelea na kazi zao ngumu pamoja na ahadi na uhakikisho kwamba watapata watalipwa kwa ajili hiyo baada ya kufa kwao. Mtalipwa katika ulimwengu ujao. Wakiulizwa tutalipwa vipi, wanajibu kwamba mtakwenda Peponi na huko mtapata mabustani mazuri yaliyojaa miti ya matunda na vijito, na kwa ajili starehe yenu, watakuwepo Mahuraraini (wanawake wa kimalaika).

Inawezekana kwamba baadhi ya watu wanaweza kuridhika na ahadi hizi lakini baadhi wanaweza wasiridhike. Wanaweza wakauliza tutaishi huko kwa muda gani. Tutapata Mahuraraini wangapi, mmoja au wanne? Itakuaje kama tukichoshwa na maisha hayo baada ya muda? Na kama wanaume wameahidiwa Mahuraraini, vipi kuhusu wanawake? Watapata nini? Wao pia wametekeleza majukumu yao ya kidini na kuteseka katika ulimwengu huu.

Ona jinsi maswali mengi yanavyokuja kwenye akili kuhusiana na Pepo na Jahannam, wazo na dhana ya malipo na Pepo tu? Hii ndio filosofia ya dini? Wale ambao wamekubali dini kwa ajili ya faida zilizoahidiwa katika ulimwengu ujao na Pepo, tatizo lao limetatuliwa na wamefanikiwa.

Malipo yoyote wanayopata ni mazuri na yenye kutosha kwa ajili yao. Na ili kufanikiwa katika maisha yajayo, wanasoma vitabu mbalimbali; wanaitafuta *Mafatih-ul-Jinan* (Funguo ya Peponi, kitabu cha Du'a) na kusoma kutoka humo du'a ambazo huwapa *Thawaab* (malipo). Lakini hilo laweza kuwa halitoshi kwa ajili yao. Hivyo wanabeba kikokotoo cha hesabu pia, kwa sababu kwa upande mwingine vilevile wanahakikisha kwamba dhambi haziepukiki kwao; wako na uhakika mno kuhusu kula riba na kufaidi ulaji wa chakula cha haramu. Hivyo wanahitaji kukokotoa matendo yao mazuri na matendo mabaya; hii ndio maana wanahitaji kikokotoa hesabu. Wanaamini kwamba kila dhambi itahesabiwa kama moja tu na malipo kwa ajili ya kila tendo jema litalipwa mara nyingi. Hivyo hukokotoa malipo kwa ajili ya matendo yao mazuri na adhabu kwa ajili ya dhambi zao, na wanakuwa na furaha na kutosheka kwa matokeo

hayo. Baada ya ukokotoaji wa kila siku matokeo mazuri yako upande wake, kwa sababu kwa kila dhambi moja kuna adhabu moja tu lakini kwa kila tendo jema, malipo (*Thawaab*) ni mara kumi. Ina maana kama mtu anafanya mema kumi katika siku moja na akatenda dhambi 100, basi majibu huwa sawa hakuna faida wala hasara. Na kama akifanya jema moja tu zaidi, amefanikiwa.

Ni aina hiyo tu ya watu wa kidini ambao huchukulia kuongezeka kwa malipo ya thawabu kama filosofia ya dini na Pepo kama lengo la dini, hawana wasiwasi kuhusu kufanya dhambi kwa vile tayari wana vikokotoa hesabu vyao. Hawaogopi kusema uwongo, kusengenya na hawajali kabisa kuhusu dhambi ndogo au kubwa na wanakanyaga haki za wengine.

Ni aina ya watu hawa wa kidini ambao wanabadilisha dhana nzima ya dini. Kama unawasilisha Uislamu kwa mtu yeyote katika muundo huu, matokeo yatakuwa ni nini? Hii ina maana kama mtu asiye wa dini akimuangalia mtu wa dini (mwenye kusali nk.), lakini kwa uwazi anafanya matendo yasiyofaa, basi itakuwa ni picha gani ya dini hii juu ya mtu asiye wa dini. Je, atavutiwa hata siku moja kuelekea kwenye dini?

## Tofauti kati ya Madhumuni na Manufaa

Madhumuni ya dini ni kinyume na yale tunayofikiria kuwa na kuyatoa kwa wengine pia. Kuna mambo mawili katika dini. Moja ni Madhumuni na pili ni Manufaa na vyote ni vitu tofauti. Katika kila kitendo kuna lengo na baada ya kila kitendo kuna matokeo ambayo unaweza kuyaita manufaa.

Wakati tunahudhuria hafla ya dini kwa ajili ya lengo, lakini wakati hafla hiyo ikiisha kutakuwa na manufaa fulani pia kama vile elimu, kukutana na watu wengine, viburudisho na mambo mengine. Haya ni manufaa ya hafla, sio lengo. Kama vile unavyokwenda kwenye Majlis, unapata chakula wakati wa mwisho. Chakula hiki sio madhumuni ya Azadari; hii ni faida ndogo ya kujiunga katika Azadari. Hivyo, kuna tofauti nyingi kati ya mad-

humuni na manufaa.

Kuna aina fulani ya watu ambao kwamba sisi wote hatuna furaha nao na tunawalaani. Lakini pengine, baadhi yetu tuko tu kama wao wakati likija suala la dini. Watu hawa wanaitwa wabinafsi (watu ambao huangalia maslahi yao tu). Tumeambiwa kukaa mbali na watu kama hawa.

Wakati mtu anapotaka kumkashifu mtu, atamuita mbinafsi ambayo humaanisha anasema kwamba wewe ni mtu ambaye hufikiria tu kuhusu wewe mwenyewe na kufanya kwa ajili ya faida na manufaa yako mwenyewe binafsi tu. Wakati tunapotaka msaada kwa mtu kama huyo, hatafurahia kutusaidia mpaka aone kuna maslahi binafsi katika kutusaidia.

Lakini huu sio ufafanuzi sahihi au tunaweza kusema sio ufafanuzi kamili wa mtu kuwa mbinafsi. Mtu sio mbinafsi tu kwa sababu hawezi kutusaidia. Chukua kwa mfano mtu ambaye ni wa dini sana na huhudumia Uislamu na wanadamu kama mtumishi, lakini hawezi kutusaidia. Kwa vile hawezi kufanya kazi yetu, baadhi ya watu wanaweza kumuita mbinafsi. Hiyo sio sahihi. Watu wenye ubinafsi sio wale ambao hawawezi kutusaidia (kwa sababu hawana uwezo wa kutosha wa kutusaidia) badala yake ni watu ambao kamwe hawafikirii kuhusu Madhumuni bali wanajali tu kuhusu manufaa.

Faida ni kitu kinachopatikana chenyewe wakati wa kukamilika kwa kazi yoyote. Kila kitendo tunachokitenda kina faida kwa namna fulani au katika muundo mwingine; na kuna madhumuni pia katika kila kitendo. Kuna mfano wa rahisi sana wa kanuni hii; tunakula chakula kila siku na kuna madhumuni katika hili. Tunakula chakula kwa sababu ni muhimu kwa ajili ya mwili wetu ili kufanya kazi zake sawasawa. Faida ya chakula hiki ni kwamba tunapata ladha ya chakula na furaha.

Sasa unaweza kuamua nani ni Mbinafsi na nani aliyeelekea kwenye Madhumuni. Wakati tukila chakula, tunaona madhumuni au faida?

Tunakula chakula kwa ajili ya furaha au kwa ajili ya kuishi? Wale ambao wanakula chakula cha kitajiri au chakula chenye viungo vingi majumbani mwao au wanaokwenda kula mahotelini mara kwa mara kwa ajili ya vyakula vilivyoungwa kwa viungo vingi, je, wanakula kwa ajili ya furaha au kwa ajili ya kuishi? Kunde na nafaka tu zinatosha kwa ajili ya kuishi. Lakini licha ya hili utaona vyakula aina mbalimbali juu ya meza. Hivyo vyakula vingi mbalimbali wakati mmoja sio kwa ajili ya kuishi, ni kwa ajili ya furaha tu, na furaha sio lengo la kula chakula, ni kwa ajili ya manufaa tu. Hii haina maana kwamba mtu anayekula kwa ajili ya furaha ni mbinafsi, huu ni mfanano uliotolewa kwa ajili kuelezea dhana ya Ubinafsi na Mtazamo wenye nia ya kuelekea kwenye dini. Furaha na vyakula mbalimbali yote haya ni neema za Allah Aza wa Jallah, kujiepusha kutokana na hivi kwenyewe ni kuzikataa neema za Allah. nukta zilizotajwa hapa ni kuhusu mtazamo au msimamo wetu ambao ni kuelekea kwenye manufaa (yaani, ladha) sio Madhumuni. Hii ndio sababu kwamba tunaishia kula vyakula vyenye ladha ambavyo mara nyingine vina madhara kwa ajili ya afya yetu lakini kwa ajili ya manufaa tunajasiri hata kuhatarisha afya zetu.

Sasa unaweza kuamua kwa urahisi ni nani ni Mbinafsi na nani ni mwenye Msimamo. Wale ambao wanakula ili wapate manufaa fulani kama furaha tu ni Wabinafsi na wale ambao hula chakula kwa ajili ya Madhumuni ni watu wenye Msimamo. Maulana Ruum amesema kwamba nguvu madhubuti za Imamu Ali (as) hazikutoka jikoni na chakula kizuri. Imamu Ali (as) alikuwa akila mikate mikavu ya shairi na zile nguvu katika mikono yake zilikuwa ni kwa sababu ya mikate ile mikavu ya shairi alikula chakula chake kwa sababu ya umuhimu wa Madumuni na sio kwa ajili ya faida yoyote au starehe.

Wamiliki wa mahoteli wanafahamu sana kwamba watu ni wabinafsi. Wanakula chakula kwa faida tu ndio maana huandalia vyakula mbalimbali tofauti vya viungo kama kuku, mikate iliyoshindiliwa nyama na mboga mbalimbali (*burger*) nk. bila ya kufikiria athari za madhara ya vyakula vyenye vikorokoro na viungo vingi. Halikadhalika pia kuna madhumuni

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:31 PM Page 10



katika kuvaa nguo na lengo ni kusitiri mwili ulio uchi na kuuhifadhi kutokana na joto, baridi na vumbi, lakini faida ya nguo ni kuonesha hadhi ya kijamii kwa sababu kwa mujibu wa desturi za kawaida hali ya nguo huakisi hadhi.

Hakuna utendaji bila ya vipengele vyote hivi; Madhumuni na Manufaa. Mtu mbinafsi ndiye ambaye siku zote hufikiria kuhusu faida ambayo sio kitu kizuri. Kwa mfano pia kuna madhumuni na manufaa katika ndoa. Chukua mfano wa mtu tajiri ambaye ana binti na mtu mwingine ambaye ana kijana wa kiume. Huyu mwenye kijana wa kiume anaweza akafikiria kwamba kama kijana wake atamuoa binti wa tajiri basi utajiri na mali yote itakuja katika nyumba yake. Kwa upande mwingine, kuna mtu ambaye ana binti na anafikiri kwamba kama binti yake ataolewa na mtu mwenye kazi nzuri na usuli wenye ufanisi, binti yake atakuwa na furaha na kuwa na ufanisi na maisha yake ya baadae yatakuwa salama. Mawazo kama hayo sio madhumuni ya ndoa. Hii ni faida ya ndoa. Mbinafsi hufikiria kama akimuoza binti yake au kijana wake kwenye familia ya kiongozi fulani wa kisiasa, wanaweza wakapata manufaa zaidi. Kuna madhumuni mawili ya ndoa, moja ni uridhishaji wa matamanio na nyingine ni uzalishaji wa familia. Sasa unaweza kuamua ni ndoa ngapi zinzfanywa kwa ajili ya madhumuni na ngapi zinafanywa kwa ajili ya manufaa; vipi watu wabinafsi wanavyofanya ndoa zao.

Pia hali kama hiyo ipo katika dini. Wale ambao wanakubali dini wanaweza kuwekwa katika aina ya makundi mawili ya watu ambao hukubali dini tu kwa ajili ya manufaa yake na wengine ambao hukubali kwa ajili ya madhumuni yake vilevile. Mtu ambaye ni mbinafsi katika kila hatua yake ya maisha atakuwa mbinafsi na dini vilevile. Kuna faida nyingi kwenye dini na anaikubali dini tu kwa ajili ya faida zake, ingawa kuna madhumuni katika dini. Wale ambao husali kwa ajili ya manufaa ni wabinafsi wakubwa mno. Wanavutiwa tu na faida. Ona jinsi wanasiasa wa nchi yetu walivyojiegemeza kabisa kwenye ubinafsi; wanasiasa walioko madarakani hawajali kuhusu haki au makosa, au iwapo ni wenye manufaa kwa ajili ya nchi

au la. Wanaangalia tu manufaa yao wenyewe. Katika siasa za ubinafsi, wamepuuza kabisa nchi na dini; wanasiasa wanatamani faida tu, popote watakapoipata. Siasa za kibinafsi zimeharibu nchi nyingi za Kiislamu; siku moja wataiharibu dini pia, kwa sababu wameikubali dini kwa ajili ya manufaa yao tu.

## Madhumuni na Manufaa ya Dini

Sasa hebu tuangalie madhumuni ya dini ni nini na faida za dini ni nini? Hebu natujaribu kujifunza filosofia ya dini na tuelewe kwa nini watu wanakubali dini? Je, kuna tofouti yoyote kati ya watu wa dini na watu wasio wa dini? Ona faida za dini. Watu wanaweza kupata faida zaidi bila ya dini pia, watu hukubali dini kwa ajili ya heshima, utukufu, fahari, hadhi, pesa na utajiri.

Wakati unapompeleka mtu ili kupata elimu ya dini, baada ya kumaliza masomo yake anarudi. Sasa ni nini anachokifanya? Atafanya kazi ama ya Imamu wa Sala Msikitini au Mhutubu wa dini popote atakapopata ujira mzuri. Watu hawafanyi juhudi ya elimu ya dini kama madhumuni; wanavutiwa na faida zake. Wanajua kwamba hii ina faida zaidi. Sasa unaweza kuona kwamba elimu ya dini iko mikononi mwa watu wabinafsi kabisa; kwa kweli vyote Dini na Dunia viko mikononi mwa watu wabinafsi.

Wale ambao wameziharibu nchi za Kiislamu na dini ni watu wabinafsi. Ni nini tofauti kati ya madhumuni ya dini na faida za dini? Kwa kweli kwetu sisi wengi wetu, madhumuni ya dini yanaishia tu kwenye Malipo (*Thawaab*); hali tulivyo ni - fuata njia ya dini ili upate *Thawaab*; funga ili upate *Thawaab*; tekeleza desturi za dini ili upate *Thawaab*; soma du’a na upate *Thawaab*; wahudumie wanadamu wenzio kwa ajili ya kupata *Thawaab*; kila kitu kwa ajili ya *Thawaab* tu.

Kama kijana akiwauliza kwa nini anapaswa kukubali kanuni za dini na kwa nini alazimike kusali, watajibu; Utapata Malipo (*Thawaab*). Kama kijana atauliza, Tutafanya nini na Malipo hayo? Wanazungumza kuhusu Hururain; huu ndio udhihirisho wa Malipo (*Thawaab*). Kisha wanauliza: Kama mwanaume atapata Hururaini, je, ni vipi kuhusu wanawake? Watapata nini kama Malipo (*Thawaab*)? Kwa sababu wakati wowote tunapofikiria kuhusu Pepo, tunaona tu kwayo kuhusu mtazamo wa mwanaume. Hakuna aliyezungumzia kuhusu Pepo ya wanawake. Vipi wanawake hawa watakavyokuwa katika ulimwengu ujao na mustakabali wao utakuwaje? Kwa nini wao wana shida? Wakati wa kusoma *Talqin* (kisomo cha mwisho cha ibada ya mazishi) tunatikisa bega la maiti na kumuambia; Sikia na uelewe kwamba Pepo ni kweli, Jahannam ni kweli, Malipo kwa ajili ya matendo mema vilevile ni kweli. Hakuna shaka kuhusu ukweli wa vitu hivi; Malipo ya *Thawaab* ni ahadi kutoka kwa Allah na kwamba haiwezi kuwa uwongo. Anaweza kusamehe dhambi zako lakini kamwe hatasahau matendo yako mazuri. Yeye sio bahili, mnyonge, asiye na uwezo au dhalimu; Yeye ni mkarimu tu. Kama akitoa Malipo ya *Thawaab* kwa wingi na zawadi ya Pepo na Hurulaini haina maana kwamba madhumuni ya dini yamefikiwa.

Lazima utakuwa umeona kwamba baadhi ya watu wamechelewa kuja kwenye Majlisi na baadhi wanakuja wakati wa mwisho na kujipatia chakula ambacho ni ratiba ya mwisho ya hafla hiyo; wanadai kwamba nao vilevile wameshiriki katika Majlisi. Lakini wameshiriki katika faida ya Azadari na sio madhumuni. Haya sio madhumuni ya dini. Haya ni manufaa tu, madhumuni ni kitu kingine. Madhumuni ya dini sio Malipo ya *Thawaab* au Pepo. Jahannam na Pepo sio madhumuni ya dini, wala uumbwaji wa mwanadamu sio madhumuni ya dini.

**Madhumuni ya dini ni nini?**

Lazima ieleweke kwamba Allah Aza wa Jallah, miongoni mwa viumbe Vyake vinavyotambulika, amewazawadia dini wanadamu tu. Hatuwezi

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 13



kusema chochote kuhusu viumbe ambao hawawezi kutambuliwa, isipokuwa Majini. Hakika dini ipo miongoni mwa Majini. Kuna viumbe Wake wengine kama vile Malaika, Malaika wakuu, wanyama, mimea na mawe, viumbe chini ya ardhi, juu yake na katika anga; kuna aina nyingine za viumbe lakini hakuna dini kwa ajili yao.

Mwenyezi Mungu amewazawadia dini wanadamu tu. Kwa nini isiwe kwa viumbe wengine? Je, dini sio muhimu kwa viumbe wengine? Kama sio muhimu, basi kwa nini ni muhimu kwa wanadamu? Hakuna taratibu ya ndoa kwa ajili ya wnyama. Hakuna taratibu za dini kwa ajili ya wanyama, ziko kwa ajili ya wanadamu tu. Mwanadamu ameelekezwa mahususi kutekeleza majukumu yake yote ya dini na kaida zake. Kwa nini? Kwa sababu dini ni njia ya maisha, kanuni za utendaji na ni uwakili wa ufalme. Hivyo, ili kujua kuhusu dini hii na filosofia ya dini lazima tuelewe kuhusu wanadamu kwanza. Dini haina maana bila ya wanadamu, kwa sababu ipo tu kwa ajili ya wanadamu.

Ni uhusiano gani unatupasa kuwa nao juu ya dini? Ili kujua kuhusu hilo, lazima kwanza tujue kuhusu wanadamu; bila ya kuwajua wanadamu mada hii itakuwa pungufu, hatuwezi kuelezea filosofia ya dini. Kwa nini dini ni muhimu kwa ajili ya wanadamu? Kuna tofauti gani kati ya mshika-dini na muasi wa dini? Ni vigumu sana kuelezea hilo kwa muda mfupi. Sio bahari moja, bali bahari saba lazima zifungiwe kwenye kikombe. Na mjadala mfupi hauwezi kutatua madhumuni hayo kwa sababu huleta maswali zaidi na mkanganyiko katika akili. Mada hizi lazima zielezewe kwa uwazi kabisa. Allah ametupa maisha haya ili tumtumikie Yeye na dini Yake, laki-ni hatuna muda kwa ajili ya aina hii ya kazi; tuna muda zaidi kwa kazi nyingine ambazo sio muhimu. Hii ina maana kwamba hatutumii muda kwa ajili ya masomo ya dini, tunatumia muda mwingi kufanya mambo ambayo sio muhimu, kipengele muhimu cha maisha yetu ni dini, ambayo kwayo tunajua kidogo sana na wala hatuvutiwi kujifunza zaidi. Katika muda huu mfupi, nitajaribu kuelezea kwamba kuna tofauti moja tu kati ya wanadamu na viumbe Wake wengine, tofauti ni kwamba viumbe wengine wameletwa

duniani hapa baada ya kuwa wamekamilishwa. Hii ina maana kwamba, hawa viumbe wengine wameletwa na Allah (s) katika umbile walilopaswa kuwa nalo hapa juu ya ardhi, wamekamishwa na Malaika kabla ya kupelekwa ulimwenguni. Lakini ni tofauti na wanadamu, wao wameletwa hapa ulimwenguni kujikamilisha wenyewe (kufanya harakati kuelekea kwenye ukamilifu). Kwa mfano, unampeleka mtoto wako shuleni kusoma. Kuna vitu vingi sana shuleni; viti, meza, na mbao za kuandikia; jengo la shule liko pale na kuna vitu vingi sana ndani ya jengo hilo; kila kitu kiko tayari. Mwalimu hakukodishwa kutengeneza meza, viti au mbao za kuandikia, lakini unampeleka mtoto wako ili kujenga tabia yake na kazi yake ya baadae. Hivyo, katika sehemu hiyohiyo; shuleni hapo, kuna vitu vingi sana, ambavyo viko kamili, na kuna vitu vingine ambavyo vinahitaji kukamilishwa. Halikadhalika, unachukua unga kuupeleka kwenye tanuri ili kuoka mkate.

Allah (s) kupitia uumbaji Wake aliumba ulimwengu Yeye mwenyewe. Allah (s) kwa uwezo Wake wa milele ameumba kila sehemu ya ulimwengu Yeye Mwenyewe. Mwanadamu ni sehemu moja ya ulimwengu huu. Nusu ya uumbaji wa mwanadamu Allah (s) ameifanya Yeye Mwenyewe na nusu nyingine aliachiwa mwanadamu mwenyewe. Uumbaji wa ulimwengu ulifanywa kwa ukamilifu na Allah (s) lakini ilipokuja kwa mwanadamu ilifanywa katika hatua mbili. Hatua moja ni ile iliyokamilishwa na Allah (s) na ya pili ni ile iliyoachwa juu ya mwanadamu mwenyewe ili kuitengeneza hatua hii. Hivyo kuna sehemu mbili za watu; moja ni *Khalq* na ya pili ni *Khulq*. *Khalq* ni sehemu ile ambayo hukamilishwa na Allah (s) ambapo *Khulq* ni sehemu ile ambayo hufanywa na mtu mwenyewe. Mwanadamu huyo ameonyeshwa njia, utaratibu umeakwisha kupangwa na vilevile vitu vya kufanyia *Khulq* vimetolewa; na kisha mtu ameambiwa kutengeneza *Khulq* katika njia ileile ambayo *Khalq* yake imeumbwa na Allah (s)

*Khalq* au uumbaji wa mtu umeelezewa katika Qur'an Tukufu na Allah (s) katika mtindo sahihi sana na fasaha. Maelezo yanaanza mwanzo kabisa

kutoka pale tulipoanza uumbaji. Tulianzisha uumbaji kwa udongo wa mfinyazi, tukapata kutoka humo zidua, kisha zidua hii iligeuzwa kuwa kwenye manii, manii yaliwekwa kwenye tumbo la uzazi, ambapo baada ya hapo iligeuzwa kuwa pande la damu ndani ya tumbo la uzazi, ambapo baada ya hapo liligeuzwa kuwa nyama na kisha tulitengeneza mwili kutokana nayo. Kisha tuliweka nyama na mifupa kwenye mwili huu na baada ya kuufunika na ngozi tuliweka roho ndani yake na kisha tukasema:

فتبارك الله احسن الخالقين

Hizi ni hatua za uumbaji kutoka kwenye udongo wa mfinyazi mpaka kwenye roho ambazo zimetajwa kwa uwazi katika Surah Tini. Baada ya kutaja hatua hizi Allah (s) anamuambia mwanadamu kwamba lazima awe muangalifu kwa sababu tumelifanya umbo lake kuwa bora sana, kamili na imara. Hii ina maana umekuwa umeumbwa kwa uzuri bora uwezekanao, adhimu na utukufu. Lakini uumbwaji wako sio ubinadamu wako badala yake uumbwaji wako ni mifupa au umbo (fremu) kwa ajili ya ubinadamu wako. Uumbwaji wako una vitu vya ubinadamu ndani yake na sasa lazima utengeneze umbile la ubinadamu wako kwa vitu hivi wewe mwenyewe. Lazima ugeuze umbo hili kwenye ubinadamu na utu wewe mwenyewe. Vipi? Jukumu hili limekabidhiwa na Allah (s) kwa binadamu mwenyewe. Jina la mafundisho hayo, kile kitu, *Khulq* ambacho mwanadamu huiweka ndani ya ukiumbe huu bora (*Khalq*) ni Dini. Dini imekuja tu kwa ajili ya lengo moja pekee, madhumuni na ujumbe madhubuti ambao ni kutufanya sisi wanadamu kweli kweli. Mtu lazima awe msanifu wa nafsi yake mwenyewe na kujenga uhai wake. Kile Allah (s) alichofanya ni fikira tu za ukweli wa mtu, binadamu halisi lazima atengenezwe na mtu mwenyewe.

Kwa maneno mengine tumewekwa tukiwa tumefichwa nyuma ya ngozi hii, na nyuma ya pazia hili la ngozi tunatakiwa kuchora picha ya kipekee. Na ni kanuni ya kawaida kwamba picha za kipekee hazifanywi au kuchorwa katika sehemu za hadhara au sehemu za umma za wazi; picha za kawaida zinaweza kufanywa katika sehemu yoyote kwa sababu hakuna neno

hata kama mtu ataiangalia wakati inapofanywa. Lakini ni wapi picha za kipekee zinafanywa na mchoraji? Huifanya katika sehemu iliyozingirwa, chumba kilichofungwa, studio ya siri. Wakati picha hii ikiwa tayari yeye huitangaza na kualika kila mtu kuja siku maalumu kwa ajili ya sherehe za kufunua pazia. Huita kila mtu ili kuona aina gani ya kazi aliyoifanya ambayo itaonekana mara tu pazia litakapoondolewa juu ya picha. Allah (s) ametoa mazingira yaliyofungwa kwa mwanadamu na katika mazingira haya yaliyofungwa, nguo, pazia limewekwa ambalo jina lake ni ngozi na vilevile lilisema kwamba mimi ni "Sitara" (*Sattara*." Tunamdhukuru Allah (s) kwa jina hili "*Ya Sattar*" (Ee! Mwenye kusitiri). Tunamuita Allah (s) kama "*Sattarul Uyoob*" (Mwenye kusitiri makosa na aibu zetu) na kasoro kubwa ambayo Allah (s) ameisitiri ni picha ambayo tunaichora chini ya ngozi hii. Allah (s) alitengeneza umbo na akatukabidhi pamoja na vitu vya kuchorea ambavyo kuanzia hapa na kuendelea itakupasa wewe mwenyewe kujitengeneza na kisha siku moja alisema siku moja pazia litaondolewa kutoka kwenye picha hii, na siku hiyo ni *Kiyamah* (Siku ya Hukumu). Moja ya majina ya Siku ya Hukumu yaliyotajwa na Qur'ani ni:
يوم طبل شر ائر ambalo maana yake siku ya kuondoa mapazia na kuondoa sitara iliyowekwa juu yetu. Lakini pazia litaondolewa kutoka kwenye vitu gani? Ni kutoka kwenye picha hizi na roho. Leo kila mtu anaonekana kama wanadamu walio sawa nyuma ya ngozi lakini katika Siku ya Hukumu pazia la ngozi litaondolewa na chochote kinachotokea nje kutoka ndani hakitakuwa sawa kwa kila mtu. Kwa hili pia Qur'ani Tukufu imetumia maneno mahususi, aya maalumu zipo kwa ajili ya hili na sura tofauti ambazo zimefichwa nyuma ya ngozi vilevile zinatajwa.

Kila mmoja wetu aliumbwa ili kujitengeneza wenyewe. Dini ni ilani ya mwongozo kwa ajili ya ujenzi wa mtu. Kila kitu katika dini na kila sehemu ya dini imekusudiwa kwa ajili ya ujenzi wa mwanadamu; lakini sehemu ya dini ambayo tumeisikia haifikii hata moja ya kumi ya upana wa dini. Tulichoambiwa ni kidogo na sehemu ya kawaida ya dini ambayo kwamba tumeshirikishwa na kuitekeleza mwaka mzima. Sehemu kubwa ya dini tumefichiwa; haikufundishwa kwetu; siri hizi hazifichuliwi. Wakati

mwingine pia watu wanasema kwamba mambo yote makubwa ya kimaendeleo ya ulimwenguni yamefanywa na watu wasio wa dini. Maendeleo yote na kupanda kwa tekinolojia kunakoonekena ulimwenguni leo, zana zote hizi za mashine za kipekee na za kushangaza, ambazo huzalishwa kila siku, zote zimeendelezwa na watu wasio wa dini. Watu wa dini hawakuzifanya hizi, zimefanywa na wale ambao amma hawana dini au wenye dini ya kisekula na imani dhaifu au kwa maneno mengine maendeleo haya hayakupatikana kwa mafundisho ya dini.ingawa leo tuna mahatibu na wahubiri ambao wanasema kwamba maendeleo yote haya yamesukumwa na mafundisho ya dini tu, lakini mbali na maneno ya wahubiri hakuna ushahidi uliopo kwa hili. Hakuna shaka kwamba dini imekuwa na siri kama hizi ndani yake, lakini kwa hakika wale ambao wamefanya maendeleo haya hawana uhusiano na dini. Kama ukiangalia katika neema hii kubwa ya umeme; mtu ambaye ameugundua alikuwa sio mtu wa dini kabisa na wala hakusukumwa au kushawishiwa na mafundisho ya dini kwa maendeleo haya; ilikuwa ni kitu kingine ambacho kilikuwa msingi wa ugunduzi huu. Halikadhalika leo tunanufaika kutokana na kompyuta; mtu ambaye amegundua na kuendeleza neema hii alikuwa hakusumwa na dini. Anaweza kuwa amechukua msukumo kutoka sehemu nyingine ile kama kwenye fizikia, mafundisho ya kisayansi nk, na vilevile ni kweli kwamba watu fulani wanapewa akili hii na Allah (s) kwamba wao wenyewe wamefanya utengenezaji na uvumbuzi huu

Swali ambalo linachomoza ni hili ni wakati ambapo maendeleo yote haya, ugunduzi na vitu vyote ambavyo tunavyiona siku hata siku za maisha yetu, vifaa tunavyotumia kujengea nyumba zetu na miji ambayo tunaishi pamoja na njia zote hizi za maisha ndani yake, kila kitu kimefanywa kwa mwongozo kutoka nje ya dini; basi ni nini faida ya dini? Kwa nini dini ilikuja kwa ajili ya mwanadamu? Wakati kila kitu kinakuja nje ya dini, hivyo dini ni ponyo la maumivu gani? Hapa ndipo tunapoambiwa dini ni kwa ajilili ya ulimwengu ujao. Hii ina maana kwamba ulimwengu utatengeneza viwanda na ulimwengu uko mikononi mwa wanasayansi na wanafikra. Mfumo wa ulimwengu utaendeshwa na wanasayansi, wanafikra, madaktari

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 18



wakulima wakubwa na wahandisi, lakini hawana cha kufanya katika ulimwengu ujao (Akhera). Ulimwengu ujao unakabidhiwa kwenye dini na ni dini ambayo itafanya ulimwengu ujao. Ulimwengu ujao hapa una maana ulimwengu baada ya kifo; na katika ulimwengu huo shughuli za dini huanza. Hili ni suala ambalo liko katika akili za watu wa kawaida. Haya ni maoni na mawazo yasiyo sahihi kuhusu dini, kwamba dini imekuja kwetu tu kwa ajili ya maisha baada ya kifo.

Dini ni ilani ya maisha na imekuja kutengeneza maisha kabla ya kifo. Chochote kitakachofanywa kabla ya kifo kitakuwa kimefanywa na dini tu, na chochote tunachofanya kabla ya kifo kitakwenda pamoja nasi katika ulimwengu ujao (Akhera). Sio kwamba tunafanya kitu kingine katika ulimwengu huu na tunapata kitu kingine katika ulimwenu ujao. Chochote tunachojenga hapa kitakwenda pamoja nasi kwenye ulimwengu ujao; yote yale yanayotengenezwa hapa yatahamishiwa katika ulimwengu ujao. Hivyo, dini imekuja kwa ajili ya maisha kabla ya kifo na baada ya kifo matokeo ya dini yatapatikana na sio kwamba dini ndio sasa itakuwa hai.

Kama dini imekuja kwa ajili ya ulimwengu huu basi vitu vyote hivi vya kiulimwengu lazima viwe vimefanywa na dini; kama simu za mkononi, kompyuta na vifaa vyake vyote lazima vitakuwa vimefanywa na dini. Je, tuweke matumaini haya kwenye dini? Dini haikukusudiwa kufanya vitu vyote hivi kwa sababu Allah (s) amemtunuku mtu uwezo, akili na vipaji mbalimbali kufanya vitu vyote hivi. Amempa mwanadamu uwezo, akili, werevu ma vipaji vya kutenda navyo hivyo pia kwa wingi sana. Mwanadamu kapewa nguvu na Allah (s) na uwezo wa kufikiri, kuelewa, kupata elimu, kukadiria vitu, kufanya vitu; uwezo wote huu umewekwa ndani ya mwanadamu na Allah (s). Kwa nini uwezo wote huu uwekwe ndani ya mwanadamu? Hii ni kwa sababu vitu fulani lazima avifanye kwa msaada wa uwezo huu. Uwezo wote huu na vipaji vilivyowekwa ndani ya mwanadamu sio uwongo, uovu au takataka; vimewekwa ndani ya mtu kwa ajili ya madhumuni na malengo fulani. Kwa mfano kama una uwezo wa kuelewa hisabati ndani yako basi kuwa na hakika kwamba uwezo huu

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 19



umewekwa ndani yako kwa ajili madhumuni fulani. Kila mtu ana uwezo uliopo ndani yake pamoja na nguvu na ukubwa tofauti. Kwa mfano wengine ni wepesi katika uhasibu, baadhi ni wazuri sana katika Aljebra, kisha kuna baadhi ambao ni wazuri katika nyanja ya umakanika au baadhi ya wengine katika sayansi na kisha baadhi ya wengine wana umakini wa kina katika nyanja nyingine. Kila mtu ametunukiwa taaluma mahususi. Ipo katika hadithi kwamba:

كلّ ميسرّ لما خلق

"Kwa kila mtu ni rahisi kufanya kile kitu ambacho kwamba ameumbwa kukifanya."

Hii ina maana kwamba kila mtu ameumbwa na Allah (s) kwa ajili ya kazi maalumu na kama ataishia kuifanya kazi hiyo atafanikiwa. Tumeumbwa kwa ajili ya kitu fulani na tunaishia katika nyanja nyingine. Na msiba huu umetokea mpaka sasa; wengi walipaswa kuwa wahandisi lakini wamekuwa madaktari na vivyo hivyo kinyume chake. Wanachuoni wengi wa dini wangelipaswa kuwa wakulima na wakulima wengi wangelipaswa kuwa wanachuoni. Kuna wafanya biashara wengi ambao taaluma yao sio biashara walipaswa kuwa kwenye taaluma nyingine na wengine wengi ambao wako kwenye nyanja nyingine wangelipaswa kuwa wafanya biashara. Kuna wengi ambao walitamani kuwa katika nyanja nyingine lakini wazazi wao wakawafanya kuwa katika nyanja nyingine. Tunaishia katika nyanja tofauti na vilevile tunafanikiwa huko lakini kama tungelichukua nyanja zile za matakwa yetu na zaidi ya hilo tukajikita juu ya uwezo wetu tungelifanikiwa zaidi. Kwa hiyo, lazima tuelewe na kutambua uwezo uliopo ndani yetu.

Moja ya mambo juu ya malezi ya watoto kwa wazazi ni kwamba lazima watambue na kufahamu uwezo uliopo ndani ya watoto wao. Kazi ya taasisi za elimu sio kuwafanya wanafunzi kukariri vitabu na masomo, badala yake kazi za taasisi, shule na seminari za dini ni kutambua uwezo uliopo

ndani ya wanafunzi. Kazi ya elimu ya msingi ni kutambua uwezo na kisha baada ya hili jukumu la sekondari na elimu ya juu ni kulea na kuza uwezo huu. Katika mfumo wetu elimu ya msngi, sekondari na elimu ya juu wote umeelekezwa juu ya kumfanya mwanafunzi kuhifadhi masomo yake; kuanzia umri wa miaka 3 mpaka 24 wote wako katika harakati za kumfanya mwanafunzi ahifadhi masomo yake. Huu sio mfumo wa elimu, kwa kweli ni mpasuko katika mfumo wa elimu. Hupaswi kumlazimisha mtoto kujifunza kwa muda fulani lakini badala yake unahitaji kumuelewa mtoto, kumchunguza mtoto kuona ni kitu gani Allah (s) ameweka ndani yake? Kazi ya elimu ya msingi ni kutambua uwezo uliopo ndani ya mtoto. Wakati akitambuliwa mkabidhi kwa mwalimu mwingine pamoja na taarifa kwamba nimemchunguza mtoto huyu na ana uwezo huu na huu ndani yake. Kisha mwalimu huyu bingwa lazima alee uwezo huu aufanye unawiri. Hivyo kwa kutumia ujuzi huu kama ukilelewa na kukuzwa sawasawa, mtu anaweza kufanya mambo mengi lakini kuna majukumu fulani ambayo kwamba Allah (s) amempa mwanadamu uwezo lakini mtu hawezi kutumia uwezo huu yeye mwenyewe. Kuna majukumu fulani ambayo kwamba Allah (s) amefanya maandalizi mengine maalumu. Mtu anaweza kufanya ukulima; kama sio leo basi ni kesho. Anaweza kujenga viwanda kwa uzoefu wake mwenyewe na msaada wa mafunzo na walimu wake. Ingawa mwanadamu amefikia hatua hii ya maendeleo kwa kuchelewa kabisa lakini hatimaye amefika. Amefanya viwanda, amefanya ukulima, amefanya njia za kusafiria katika anga, ameingia ndani ya atom. Kwa upande mwingine ameingia katika chembechembe ndogo sana ambapo kwa upande mwingine amefikia kwenye galaksi. Uwezo huu uliwekwa ndani ya mwanadamu na Allah (s) na kwa hiyo chochote kinachotokea nje ya dini vilevile hutokea ndani ya uwezo na nguvu alizopewa mtu na Allah (s) na kwa hiyo vitu hivi vilevile viko ndani ya maeneo ya dini tu. Hatupaswi kufikiria kwamba chochote kile kinachofundishwa katika shule za Kiarabu ni dini na chochote kinachofundishwa katika vyuo vikuu havina makosa. Usije ukachukua ushauri kama huo hata kwa bahati mbaya. Bali badala yake kile ambacho kinafundishwa katika shule za dini (Madrasa) ni ufafanuzi wa maneno ya Allah (s) wakati ambapo kile kinachofundishwa

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 21



ka vyuo vikuu na picha ya mambo ya Allah (s). ni kitu gani anachojifundisha pale? Anajifundisha Fizikia na kemia; ni nini kazi ya fizikia na kemia? Kazi yake ni kuchunguza na kufichua ulimwengu huu wa maumbile. Hivyo nani aliyeumba haya maumbile? Haya yameumbwa na Allah (s). hii ina maana kwamba Allah yule yule ambaye aliiteremsha Qur'ani vilevile ameumba ulimwengu huu; hivyo mwanadamu amekuwa akishughulika katika kuielewa Qur'ani.

Wote lazima wafahamu bila kujali mmoja kukaa katika shule ya Dini au kufundisha; au mmoja katika chuo kikuu ambaye anafundisha au anasoma kwamba kama chochote anachojifundisha kinalenga kupata faida za kidunia, basi kama anajifundisha Qur'ani haitahesabiwa kama dini. Kwa upande mwingine kama anajifundisha sayansi kwa lengo la kuelewa uhalisia wa viumbe wa Allah ulimwenguni na kisha akawakilisha kwa wanadamu; basi anafanya hivyo kwa ajili ya dini. Sio kwamba tunafanya kitu kingine na kisha tunaweka bango la alama ya kitu kingine. Leo mabango ya Dini yanawekwa kwenye shule za dini (Madrasa) lakini kinachofundishwa humo ndani ni ugaidi. Hii sio dini, kwamba wanakaa ndani ya shule ya dini kufundisha masomo ya ugaidi. Kupanda mbegu za chuki miongoni mwa wanadamu. Hii sio dini; basi dini ni nini? Dini haikuja kupanda miba, imekuja kupanda maua na maua hayo lazima yapandwe na kulimwa kwenye shule hizi za dini (*Madrasah*). Nuru lazima itoke kutoka kwenye shule za dini, manukato lazima yaenee kwenye hewa kutoka kwenye shule hizi, upendo na umoja lazima uje kutoka kwenye shule hizi, lakini kinyume chake kinachotokea ni tofauti kabisa. Hivyo chochote kinachotokea kwenye bango la alama ya dini sio lazima kiwe dini. Ni madhumuni na malengo ndiyo yatakayoamua na kusema iwapo ni dini au nje ya dini.

Allah (s) ametupa uwezo unaohitajika na anatutaka sisi tufikie hatua ile ambako Allah (s) anatutegemea sisi kufika. Angalau mwanadamu amelea uwezo huu na amefikia hapa. Mitume hawakuja kwa ajili ya kuweka viwanda; hatupaswi kuwa na matumaini haya kutoka kwa Mitume. Kama

wangelitaka wangeweka viwanda vikubwa mno. Kama Mitume wangeweka viwanda vya nguo, wangetengeneza nguo ambazo zisingechakaa mpaka Siku ya Kiyama. Wangeweza kufanya hivyo lakini hawakufanya badala yake wao wenyewe walikwenda sokoni kununua nguo. Leo chochote kile kinachofanywa kwa msaada wa maendeleo ya viwanda, Mitume wangeweza kufundisha watu kujenga viwanda na wangepata faida kubwa kutokana navyo; lakini walijizuia kufanya vitu hivi. Tende, chakula na mkate ambao watu wengine walikuwa wakila Mitume nao walikuwa wakila vyakula hivyo hivyo. Basi kwa nini Allah (s) aliwapa vyeo Mitume na Maimamu watukufu Maasumin (as)? Allah (s) amewafanya wawajibikaji kwa ajili ya jukumu ambalo mwanadamu hawezi kulikamilisha kwa uwezo aliopewa. Ni jukumu gani hilo? Jukumu hilo lilikuwa ni kumgeuza mtu kuwa mwandamu wa kweli. Mtu anaweza kutengeneza kompyuta lakini wale ambao wanatengeneza kompyuta wanaweza wasifanikiwe katika kumtengeneza mwanadamu wa kweli. Kama una shaka na maneno yangu, basi nenda katembelee Japan. Japan wanatengeneza kompyuta na kiongozi wa tekinolojia; lakini kiongozi huyo huyo wa tekinolojia yu duni mno katika itikadi ambazo anapata kutoka kwenye kompyuta na husujudu mbele ya sanamu liliotengenezwa kwa mikono. Mtu huyu ambaye amekaa juu ya kilele cha tekinolojia yuko juu ya nukta ya sifuri ya itikadi.

Kwa nini Mitume walikuja? Hawakuja kumchukua mwanadamu kwenye kupanda kwa tekinolojia badala yake wamekuja kumfanya mwanadamu afanye safari ya kupanda katika tekinolojia. Hii ni kwa sababu uwezo unaohitajika kwa ajili ya tekinolojia upo ndani ya kila mtu na Allah (s) vilevile amemsukuma mwanadamu kwenye njia hii ambako yeye mwenyewe anaweza kufikia mafanikio haya. Siku moja ataingia ndani ya atom na siku nyingine ataingia ndani ya galaksi. Lakini njia ambayo mwanadamu hupata kumpotoshwa mbali mno na hana uwezo wa kuja kwenye njia ile ambayo ni ngumu sana ni njia ya ubinadamu ambako mwanadamu anapaswa aje lakini hana uwezo wa kuja yeye mwenyewe. Watu wote hawa ambao wamekuwa wanatambulika lazima wawe ni binadamu. Madaktari lazima wawe binadamu, wahandisi lazima wawe

binadamu, wanasayansi lazima wawe binadamu, na wanachuoni hawa (Ulamaa) lazima vilevile lazima wawe binadamu. Kuna usemi katika Kifurusi ملاشدن چہ آسان آدم شدن چہ مشکل ambao humaanisha kwamba kuwa mwanachuo ni rahisi sana lakini kuwa binadamu ni vigumu sana. Imamu Khomein (r.a) alikuwa akisema kuhusu usemi huohuo kwamba ملّا شدن چہ مشکل آدم شدن چہ محال ؟ ambao maana yake ni kwamba kuwa mwanachuo ni vigumu sana na kuwa binadamu haiwezekani, Allama Iqbal (r.a) vilevile alisema hivyo hivyo:

> "Ni bora kuwa binadamu kuliko kuwa Malaika lakini juhudi iko zaidi katika hili."

Haichukui juhudi kubwa kuwa Malaika. Inatosha kuwa Malaika kwa kutafuta pango au kuifanya nyumba yako kama pango; chukua mkeka wa kusalia, birika la maji ya kutawadhia, tasbihi na weka mtu atakayekupa chakula kupitia dirishani kisha unaweza kujishughulisha wakati wote katika sala, usomaji wa du'a na utaona baada ya miaka mitano utabadilika kuwa Malaika. Lakini kwa maana hii hii, kukaa ndani ya chumba kilichofungwa huwezi kuwa binadamu. Anaweza kuwa Malaika lakini kuwa binadamu lazima aje ndani ya jamii na ustaarabu. Ili kuwa binadamu lazima atekeleze vyote, uhaiba na halikadhalika majukumu ya kijamii. Kuwa binadamu ni vigumu sana na kuna shida nyingi na misiba juu ya njia hii ya kuwa binadamu wa kweli (kwa maana ya – utu).

Jukumu rahisi limewekwa na Allah (s) juu ya kila mtu. Unaweza mwenyewe kutengeneza ndege, kompyuta, nk. kwa sababu hivi ni rahisi sana kuvitengeneza hivyo lazima uvitengeneze mwenyewe. Kuna baadhi ya kina mama ambao huwadekeza sana watoto wao kiasi kwamba wanafanya kila kitu wao wenyewe kwa ajili ya watoto wao. Ni uonevu juu ya mtoto kwa sababu kiasi mtoto anavyokua na kuanza kukuza uwezo, mtoto lazima afundishwe kufanya vitu fulani yeye mwenyewe; kama kula chakula, kunywa maji, kuvaa viatu nk.

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 24



Allah (s) hakumdekeza mwanadamu kiasi hicho badala yake alisema kwamba lazima utafanya vitu vyote hivi. Mwnadamu akasema nahitaji trekta kwa ajili ya kulimia, Allah (s) akasema utalitengeneza mwenyewe; kama huwezi kulitengeneza leo utalitengeneza kesho. Tunahitaji ndege kwa ajili ya kusafiria; Allah akasema jaribu na uitengeneze mwenyewe na ilitengenezwa na mwanadamu. Tunahitaji kompyuta, nishati ya nyukilia, nk. Allah akasema nimekupeni uwezo na siwezi kusaidia zaidi ya hili. Unatumia akili zako na utaweza kufanya yote haya; na hii ilikuwa kweli kwamba mwnadamu alifanya vitu vyote hivi. Tuliambiwa kufanya mafanikio yote haya ya kitekinolojia sisi wenyewe ili kwamba uwezo wetu uweze kukua na kung'ara.

Kitu kingine ambacho mwanadamu anapaswa kufanya na ambacho kwamba Allah (s) amefanya maandalizi maalumu, ambayo kwamba ilani ilihitajika; kwa ajili ya tekinolojia hatuhitaji ilani, mwalimu tu alitosha. Lakini kwa ajili ya jambo hili kubwa na la heshima iliani ilihitajika, na pamoja na ilani hii mwalimu anahitajika, na pamoja na mwalimu mkufunzi vilevile anahitajika na pamoja na mkufunzi kiongozi na mlinzi vilevile alihitajika. Ilikuwa ni kwa ajili hii Allah (s) aliifanya Qur'ani kama ilani, akamfanya Mjumbe (saw) kama mwalimu na mkufunzi; na akawafanya Maimamu (as) kama viongozi na walinzi ili waweze kukifanya kitu hiki kigumu kifanyike kwa wanadamu. Hiki kilikuwa ni nini? Ilikuwa kwamba lazima wachukue mifupa hii, umbo hili kuelekea kwenye ubinadamu.

Haiwezekani kufukia hadhi ya ubinadamu bila ya Mitume na dini. Tumeyaweka mategemeo haya kutoka kwenye dini kwamba imekuja tu kwa ajili ya kupata malipo (Thawaab). Tumeifanya filosofia hii ya dini kama ni malipo. Simamisha swala na kutakuwa na malipo, funga swaumu kwa ajili ya malipo, toa Khums kwa ajili ya malipo. Nazungumzia kuhusu wale ambao wafanya yote haya. Kuna baadhi ambao hawatekelezi wajibu wao, kwanini? Hii ni kwa sababu wameafundishwa kwamba utekelezaji wote huu wa matendo haya ni kwa ajili tu ya malipo; basi sawa kama akikosa kwenye baadhi ya hayo, kile anachokosa ni baadhi ya malipo. Kwa

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 25



mfano kama mtu akiambiwa kufanya kazi fulani kwa siku moja na atapata dola moja mwisho wa siku. Yeye anasema sina haja ya kufanya kazi hiyo kwa sababu dola moja sio kiasi kikubwa, naweza kupitisha usiku wangu bila hii.

Uzembe katika dini, kutokujali kuhusu dini, kutokuwa tayari katika dini, kutokutoa umuhimu katika dini yote haya ni kwa sababu filosofia ya dini imeelezwa bila usahihi na kutia shaka. Jiografia yote na ramani ya dini imechezewa. Kama sitoki Tehran na ninaambiwa kuchora ramani ya Tehran nitachora nini? Utashangazwa baada ya kuangalia ramani hii na kusema kwamba hii sio Tehran. Hii ni kwa sababu unayo ramani iliyochora na mtu ambaye haifahamu Tehran. Tunatakiwa kuchora ramani za miji ambayo tunaijua lakini kama hatukuitembelea hatutaweza kuichora sawasawa. Kama tunavyojua kuhusu Haiti baada ya tetemeko la ardhi kwamba iko karibu na Amerika. Hii imeelezewa na vyombo vya habari, lakini kama tungetakiwa kuchora ramani ya Haiti kabla ya tetemeko hili tungeiweka Haiti sehemu fulani katika Afrika kwa sababu ina wenyeji weusi. Huu ndio ujinga na uchanga wakati ramani zinapochorwa kwa kuangalia rangi au hali ya nje, basi kitu kianchotokana na Afrika kitatua Amerika na kinyume chake.

Wale ambao hawana ujuzi wa roho na ukweli wa dini wakati walipoiwasilisha dini katika jamii waliiharibu ramani ya dini; walifanya juu yake kuwa chini na chini yake kuwa juu. Waligeuza kanuni kuwa utendaji wa baadae wakati ambapo utendaji ulibadilishwa kuwa kanuni; misingi imefanywa kuwa kuta na kuta kugeuzwa kuwa misingi, matokeo yake ramani yote ya dini ikavurugika. Kwa nini Pakistan inapatwa na hali hii ya migogoro leo? Na hilo pia kwa mikono ya watu wa dini. Hii ni kwa sababu ramani ya dini imeharibiwa kabisa; jinsi unavyozidi kuetekeleza dini hiyo uharibifu utaongezeka zaidi. Jinsi unavyozidi kusisitiza juu ya dini ambayo ramani yake imeharibiwa itodorora zaidi. Jinsi majaribio yanavyozidi kufanywa kurekebisha matatizo uharibifu huongezeka zaidi. Kwa hiyo, kwanza rekebisha ramani ya dini na ifanye katika hali ile ambayo iliwasil-

ishwa na Allah (s).

Wanadamu wamekuja katika ulimwengu huu kujikamilisha wenyewe na sio katika muundo uliokamilika. Kama unaweza kuelewa nukta hii ya msingi, majadiliano zaidi yatakuwa wazi kwako. Isipokuwa kwa Mitume na Maimamu Maasum (as), hakuna mtu aliyekuja katika muundo wa usahihi na ukamilifu katika ulimwengu huu. Wote tumekuja hapa kujikamilisha wenyewe na tunajikamilisha wenyewe katika ulimwengu huu. Allah (s) amewaleta wanadamu kwenye ulimwengu huu katika muundo wa umbo au rangi; kama tunataka kuibadilisha kuwa kwenye jengo kubwa, tunaweza kufanya hivyo kwa kutumia umbo. Hivyo mwanadamu ni kama fremu tupu na mpaka tuijaze kwa vitu fulani, vinginevyo haina maana sana. Kama fremu ikikaa wazi kwa muda wa mwaka mmoja, italiwa na mchwa na itakuwa vumbi.

Hivyo, Allah amewaleta wanadamu kwenye ulimwengu huu ili kujigeuza wenyewe kuwa binadamu. Alileta tu fremu ya mwanadamu, lazima tuikamishe; tuwasanii wa sisi wenyewe na watengenezaji. Mwili wetu ni fremu tuliyozawadiwa na Allah (s). Lakini hatuwezi kufanya kitu chochote na fremu hii mpaka tuwe na nyenzo, nyenzo ambayo hujengea wanadamu. Nyenzo hiyo ni dini. *Usool-e-din*, *furoo-e-din*, haki za kimadili, *Halal* na *Haram*, adabu, mwenendo wa Mtume (*Sunnah*), majukumu ya kidini nk. ni mambo ambayo hujaza fremu hii na kumfanya binadamu halisi kutokana na mtu. Tuna tabia mbaya. Kwa kawaida, tunawadanganya wengine na kudanganywa na wengine pia. Wanasiasa hawa wanatudanganya, serikali inatudanganya, wanachukua kura zetu na kutusahau. Dini inasema usimdanganye mtu yeyote na usidanganywe na wengine, usiwe dhalimu au mkandamizaji, kuwa dhalimu ni hatia na kuwa mkandamizaji pia ni hatia.

Lazima utakuwa umewaona watu wakipamba nyumba zao kwa matunda bandia yaliyotengenezwa kwa plastiki au vitu vingine. Wakati tukiviangalia huonekana kama asilia. Vivyo hivyo, baadhi ya watu matajiri hupamba nyumba kwa wanyama bandia na ndege, kama simba. Lakini hakuna

mtu anayemuogopa. Kama ukienda nyumbani kwa mtu huyo, utakaa pale na hutaogopa kwa sababu unajua kwamba hiyo ni ngozi tu ya simba, sio simba mwenyewe. Hivyo, kama ambavyo huogopi ngozi ya simba, hupaswi kuogopa ngozi ya mwanadamu pia. Kwa sababu kuwa na ngozi ya mwanadamu haina maana kwamba kila mtu ni binadamu. Usijifanye mwenyewe mjiga.

Hivyo, muundo wa mwandamu ni fremu, maada ambayo huijaza fremu hii na kumfanya binadamu inaitwa dini; wakati mtu akifuata dini atakuwa mwanadamu kamili. Hivyo, dini sio biashara ya mkopo, yote ni ya pesa tasilimu; toa kwa mkono mmoja na ichukue kwa mkono mwingine. Fanya kazi leo na pata malipo leo hii yenyewe. Wakubwa zetu wamesema kwamba vipi dini ambayo haiwezi kufanya ulimwengu wake, imfanye mtu kuwa wa Akhera? Kama mtu hawezi kusaidia wengine kabla ya kufa, kitu gani atafanya baada ya kifo chake?

Kama nikikuambia kukaa ndani ya gari moshi na kukuambia kwamba gari hili halitakwenda Hyderabad lakini litakwenda zaidi ya Hyderabad, kwa hakika utaniuliza vipi gari ambalo halitakwenda hadi Hyderabad liende zaidi ya hapo? Dini ambayo haiwezi kumuangalia mtu mpaka kufa kwake haiwezi kunufaisha kifo chake wala kukamilisha madhumuni ya kifo, basi nini maana ya dini hii baada kifo?

Imetajwa katika hadithi kwamba “Ulimwengu ni shamba kwa ajili ya Akhera.” Ina maana kwamba ulimwengu huu ni wa muundo wa Akhera. Chochote utakachopanda hapa, ndicho utakachovuna. Sio kweli kwamba hakuna tofauti kati ya mtu wa dini na mtu asiye wa dini. Simba aliyeko porini na yule aliyeko katika varanda ya nyumba ya tajiri sio sawa. Kuna tofauti kubwa kati yao. Katika chumba iko ngozi tu ya simba; katika pori ni mnyma pori, mnyama mkali. Mtu asiye wa dini ni kama simba aliyeko porini wakati ambapo mtu wa dini mbinafsi ni kama simba wa bandia; ni ngozi ya mwanadamu lakini ndani yake imeshindiliwa nyasi kavu tu.

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 28



Wakati ambapo, mtu wa dini wa kweli ana aina ya roho ya uchaji ndani ya ngozi yake ya binadamu na anatekeleza majukumu na wajibu wake wote wa dini; mtu asiye na dini ni mtu muovu, kaidi na duni, hatuwezi kumwita bianadamu. Qur'ani tukufu imezungumza kuhusu watu kama hao:

﴿ أُولَٰئِكَ كَالْأَنْعَامِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ ۚ أُولَٰئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿١٧٩﴾ ﴾

**"Hao ni kama wanyama bali wao ni wapotevu zaidi." 7:179**

Sasa ni wazi kwamba madhumuni ya dini ni kumfanya mtu kuwa mwanadamu wa kweli. Chochote tufanyacho, asubuhi na jioni, matedno yetu yanajenga na kukamilisha uhai wetu; sisi ni watengenezaji wenyewe. Wakati tunapojenga jengo, hakuna tofali linalotupwa, liwe limepinda au limenyooka. Lakini, kama tofali limepinda na ukuta nao utapinda pia; kama tofali limenyooka na ukuta nao utanyooka. Hivyo kitu chochote tunachosema au kufanya hakitupwi.

﴿ فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٨﴾ ﴾

**"Basi anayetenda chembe ya wema, atauona! Na anayetenda chembe ya uovu atauona!" (99: 7-8)**

Pamoja na msaada wa harakati hizi tunajitengeneza wenyewe na kutengeneza uhalisia wetu; wote wale ambao wanafuata dini, halikadhalika na wale wasiofuata dini. Kama unafuata dini sura yoyote ambayo itakamilishwa itakuwa ya mwanadamu; bila ya dini, itakuwa si ya binadamu na itakuwa kama ngozi ya mwanadamu tu. Malipo (*Thawaab*) sio madhumuni ya dini yetu, bali filosofia ya Malipo (*Thawaab*) ni kufuata dini. Madhumuni ya malipo (*Thawaab*) ni kufuata dini na uwe mtu wadini wa kweli na kupata ubinadamu.

Chukua mfano wa mama yako, ni kitu cha kawaida sana na utakuwa umekiona katika kila familia. Umri wa miak 3 mpaka 5, mtoto anakuwa

mwenye kujiamini sana, anataka kula chakula mwenyewe, kuvaa nguo mwenyewe na wakati mwingine anaweza kuwa msumbufu sana kiasi kwamba hukataa hata kula chakula.

Anashindana na mama yake tu. Sio na watu wa nje na ni mama yake tu ambaye hupata shida yote ya kumlea na kuvumilia shida pamoja naye. Anakataa kunywa maziwa na kula chakula lakini kamwe mama hamuadhibu. Kama angelikuwa ni baba pahala pa mama, amgelimchapa kibao. Lakini mama hatafanya kama hivyo. Atamuambia mtoto kama hali chakula, atakila yeye. Lakini kamwe hatakula bila yeye kwa sababu ni mpole na mwenye huruma. Kama mtoto atalia usiku, baba atakasirika na kufoka akisema mtupe nje kama anatusumbua. Lakini mama hatakasirika; hii ndio maana cheo cha mama ni cha juu kuliko cha baba; mwishowe, mama anamtisha mtoto kwamba kama hanywi maziwa, ataondoka nyumbani hapo. Lakini mtoto bado hanywi maziwa, hajali vitisho hivyo hatimaye, mama anamuambia mtoto kama akinywa maziwa atamnunulia doli na anakubali kunywa maziwa.

Sasa kama utamuuliza mtoto yule kwa nini anakubali kunywa maziwa, atasema kwa ajili doli; lakini mama atasema kwamba anampa chakula ili kumfanya aishi. Vivyo hivyo, Allah (s) ameahidi malipo kama ukifuata dini. Sali na utapata malipo (*Thawaab*) na Pepo pamoja na mito ya asali na matunda kama zabibu nk. madhumuni ya malipo ni mwongozo kutoka kwa Allah (s), mvuto wa kufanya matendo mema ambayo hutusaidia sisi kuwa wanadamu halisi, na hiyo ndio maana Allah (s) ametuahadi malipo makubwa kama hayo. Na ahadi ya Allah (s) haiwezi kuwa ya uwongo. Wakati ukisali na kusoma Qur'ani, bila ya shaka kutakuwepo na malipo fulani kwayo.

Kiakili tuwachanga. Tunasali kwa sababu ya Pepo, kusoma Qur'ani kwa ajili ya Pepo na hata kufanya Azadari kwa sababu ya Pepo. Tunaamini katika *Usool-e-deen* na *Furoo-e-deen* kwa ajili ya Pepo. Lakini kuna madhumuni ya dini na hayo ni kutufanya sisi kuwa wanadamu wa kweli.

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 30



Madhumuni ya kuumbwa wanadamu ni kurudi kwa Allah (s).

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلْإِنسَٰنُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلَٰقِيهِ ﴿٦﴾ ﴾

**“Ewe Mtu! Hakika wewe ni mwenye kufanya bidii kwa Mola Wako, basi utamkuta.” (Surah Al Inshiqaaq - 84:6)**

Kukutana na Allah (s) ndio madhumuni ya kuumbwa wanadamu. Kupitia dini, mtu anakuwa mwanadamu halisi anamkuta Allah (s). mambo yote mengine, kama Pepo pamoja na mito yake ya asali na miti ya matunda, ni kwa ajili ya mvuto tu.

Sasa watazame watu ambao imani zao zilikuwa na nguvu sana zenye mvuto sana kiasi kwamba Allah (s) aliwateua kuwa Maimamu wetu. Sio kwamba kulikuwa watu wateuliwe kama Maimamu ndipo basi Allah (s) akawateuwa Maimamu; sivyo, walistahiki hilo, Allah (s) ameona kitu ndani yao. Shukurani kwa Allah kwa kututunuku dini kubwa kama hii chanzo cha kuhubiria kama hiki, Maimamu kama hawa na elimu ya dini.

Hata kama tukimshukuru Allah kwa ajili ya maisha yetu, haitatosha. Tazama, alivyosema Amirul Muminin (as):

**إلهى ما عبدتك خوفا من نارك ولا طمعا فى جنتك**
**ولكنى وجدتك أهلا للعبادة فعبدتك**

“Ewe Mola wangu! Kamwe siswali kwa sababu ya kuogopa Jahannam yako. Wala siswali kwa uroho wa Pepo. Nasali kwa sababu unastikiki kuabudiwa.” *(Ghurar ul Hikam)*

Kama usingeumba Jahannam na Pepo, au ufunge milango ya Jahannam na Pepo, au useme kwamba sitapata sehemu katika Pepo, hata hivyo Ali ataswali, kwa sababu Pepo sio madhumuni yangu, madhumuni yangu pekee ni Wewe. Wewe ndiye madhumuni ya swala zangu, kamwe siswali

kww ajili ya manufaa. Pepo vilevile ni moja ya viumbe vya Allah (s), vipi kiumbe cha Allah kiwe ndio madhumuni ya mwisho ya kiumbe kingine. Madhumuni ya swala zangu ni kukutana Wewe. Pepo ni kiumbe cha Allah (s) na mwanadamu pia ni kiumbe cha Allah (s), lakini miongoni mwa vyote mwanadamu ana cheo cha juu sana. Mwanadamu ni kiumbe kitukufu zaidi cha Allah (s).

Sasa, fikiriria unajenga nyumba nzuri sana ya kuishi. Je, nyumba hii ni kwa ajili yako au wewe ni kwa ajili nyumba hii? Je, umejenga nyumba hiyo kwa ajili yako au umeumbwa kwa ajili ya nyumba hiyo? Hivyo Pepo imeumbwa kwa ajili yetu, hatukuubwa kwa ajili ya Pepo. Madhumuni ya kuumbwa wanadamu sio kwa ajili ya Pepo, bali Pepo imeumbwa kwa madhumuni ya wanadamu waishi humo. Kama mwanadamu anakuwa binadamu wa kweli lakini (ikatokea kwamba) haendi Peponi, itakuwa ni huzuni kwa Pepo na sio kwa wewe.

Kuna msemo katika hadithi kwamba kila mtu ana mapenzi na Pepo lakini Pepo ina mapenzi na Salman Farsi (r.a). Kila mtu anaingojea siku ambayo wataingia Peponi, na Pepo inangojea siku ambayo Salman Farsi (r.a) atakuja na kuingia Peponi. Hivyo kupata Pepo sio madhumuni ya kuumbwa wanadamu; bali kukutana na Allah ndio madhumuni ya kuumbwa wanadamu. Na ili hilo lipatikane anahitaji kuwa mwanadamu kamili. Anakuwa mwanadamu kamili ili kukutana na Allah (s) kwa kupitia tu katika dini. Ili kuwaleta watu kwenye dini, kuna vivutio vyingi. Hivi ni ahadi zilizowekwa na Allah (s) na ni za kweli na zote zitatekelezwa.

Allah (s) ametupa nafasi nyingi ili tupate malipo (*Thawaab*); kila kazi nyepesi ina malipo (*Thawaab*). Kumridhisha Allah hupatisha malipo (*Thawaab*), kusalimiana kuna malipo. Kama kutoa salamu tu kwa mtu hutupatia malipo kiasi hicho, basi je, ina maana kwamba lazima tuwe tunasalimiana mchana kutwa? Kupata malipo ni rahisi. Kuna mifano mingine mbalimbali kama kumsaidia mtu kuvuka barabara utapata malipo, kumpa mnyama chakulia hupatisha malipo, kuwapa maji wenye kiu kuna

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 32



malipo. Kuna njia nyingi vilevile za kupatia malipo kutokona na matendo madogo na mepesi. Lakini kupata malipo kusiwe ndio makusudio yetu pekee.

Mwanadamu hakuumbwa kwa ajili ya Pepo; bali Pepo imeumba kwa ajili ya wanadamu. Mwanadamu ni mkubwa na wa hali ya juu sana. Allah amewaumba wanadamu kwa ajili Yake tu. Hii ndio maana hakusema AL **INSANU LILJANNA.** Bali siku zote amesema, **AL JANNAHO LIL INSANI** na akasema:

﴿ ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَٰبَتۡهُم مُّصِيبَةٞ قَالُوٓاْ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيۡهِ رَٰجِعُونَ ١٥٦ ﴾

**”Sisi sote tumetoka kwa Allah na kwa Allah tutarejea.”2:**

Mwanadamu ni kwa ajili ya Allah tu. Hakuna mashukio mengine mbali na Allah.

## Falsafa

Kuna baadhi ya watu ambao hutumia fedha zao ili kupata umaarufu; kuna watu ambao hutumia umaarufu wao ili kupata fedha. Watu kama hao wana uoni wao wenyewe kuhusu Pepo. Kwa mabahili, Pepo ni utajiri. Kwa wabinafsi, Pepo maana yake ni kuwa mashuhuri, picha zake huchapishwa kila mahali na watu humuita kwa vyeo. Lakini kuna bustani maalumu na mahususi ambayo Allah (s) ameiita Pepo:

﴿ يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفۡسُ ٱلۡمُطۡمَئِنَّةُ ٢٧ ٱرۡجِعِيٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةٗ مَّرۡضِيَّةٗ ٢٨
فَٱدۡخُلِي فِي عِبَٰدِي ٢٩ وَٱدۡخُلِي جَنَّتِي ٣٠ ﴾

**“Ewe nafsi iliyotua! Rejea kwa Mola wako hali ya kuwa radhi na umeridhiwa! Basi ingia katika waja wangu. Na ingia katika Pepo yangu.” (Surah Al Fajr; 89: 27-30)**

Hii sio Pepo ya mabustani, matunda na vikonyo; ni Pepo ya Allah (s), maana yake ni sehemu ya kukutana na Allah (s). Wakati ukienda kukutana na mkubwa fulani, anaweza kuwa nyumbani, lakini anaweza kuwaelekeza watumishi wake wakuambie usubiri katika varanda, na kukupa matunda, vinywaji, chai nk. Kuna baadhi ya watu ambao watasema kwamba ingawa hatukumkuta, kwa sababu huenda alikuwa na shughuli nyingi lakini angalau tumekula tukashiba. Mtu mmoja hujinadi kwamba alikunywa bilauri kumi za sharubati, mtu mwingine hujinadi kwamba amekunywa chupa ishirini za vinywaji baridi, mtu wa tatu anasema kwamba amekula bisikuti nyingi na wa nne anasema amekula ndizi nyingi. Lakini kuna mtu ambaye amekaa kwa huzuni sana. Hakuja hapa kula na kunywa bali amekuja hapa kukutana na mtu huyo mwenye nyumba.

Vivyo hivyo, kuna baadhi ya watu ambao Allah (s) amewashughulisha na matunda kwa sababu hataki kukutana nao. Ni njia nzuri ya kuwaepuka; hawatahuzunika na wakati huo huo wataijua sehemu Yake. Lakini kuna baadhi ya watu ambao Allah hawapi chochote kwa sababu wamekuja tu kukutana Naye; usiwazuie popote, sio katika varanda wala katika chumba cha chakula, waache waje moja kwa moja mpaka Kwangu.

﴿ فَأَمَّآ إِن كَانَ مِنَ ٱلْمُقَرَّبِينَ ﴿٨٨﴾ فَرَوْحٌ وَرَيْحَانٌ وَجَنَّتُ نَعِيمٍ ﴿٨٩﴾ ﴾

**Basi akiwa miongoni mwa waliokaribishwa. Itakuwa ni raha, na manukato, na Bustani zenye neema. (Surah Waqia – 88-89)**

Yaani wale ambao ni wapenzi sana kwa Allah hawapo kwenye pepo, bali wao wenyewe ni pepo.

Je, hatulioni hili katika ulimwengu huu wenyewe? Katika baadhi ya mikusanyiko unajihisi kama uko mbinguni. Fikiria baba anakwenda ng'ambo na anakaribia kuondoka wakati chakula kinaandaliwa. Sasa ni kipi watoto watafanya? Watakwenda kumsindikiza baba yao au watakula chakula badala ya kusindikiza? Kama ni wanadamu halisi, watasema kwamba baba

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 34



anaondoka sasa, na kesho hatakuwepo hapa, lakini chakula kitakuwa pale kila siku. Lakini kama ni walafi na wanaishi ili wale watasema muache aende, sisi ngoja tufanye kazi hii kwanza.

Hivyo usiulize kuhusu tofauti kati ya watu wa dini na wasio wa dini. Kuna tofauti kubwa, usifanywe mpumbavu. Usiulize kuhusu tofauti kati ya simba bandia katika varanda na simba aliyeko porini. Tofauti sio katika ngozi; ngozi ni sawasawa. Lakini simba sio kama ngozi. Vivyo hivyo, ubinadamu sio kuhusu ngozi. Kama ukiangalia kwenye ngozi za wote; watu wa dini na wasio wa dini, utaona kwamba ziko sawa; kuna tofauti katika muonekano.

Maana ya hili ni rahisi sana. Tofauti ni kubwa na ya wazi kama mbingu na ardhi. Mmoja ni mwanadamu katika hali halisi wakati ambapo mwingine hayuko hivyo. Tofauti kubwa iko kati ya mtu wa dini na asiye wa dini. Ni biashara ya tasilimu, sio biashara ya mkopo. Allah (s) kamwe hakusema kwamba kila kitu kitakuwa wazi. Miongoni mwa sifa nyingi za Kiyama, zimeitwa:

﴿ يَوْمَ تُبْلَى ٱلسَّرَآئِرُ ۝٩ ﴾

**Siku zitakapofunuliwa siri. (Surah Al Taariq- 86:9)**

Hivi sasa, tunajitengeneza wenyewe; tumekuja hapa kujikamilisha wenyewe, Allah hakutuleta kama wakamilifu. Leo ngozi inatupotosha; imetufanya wajinga. Hata tunaamini kwamba wao ni binadamu, wale ambao wamejaza majani makavu ndani ya ngozi zao. Ngozi ambayo ina mwongozo ndani yake ni mwanadamu halisi. Lakini, Siku ya Kiyama, wakati kamba zitakapoondolewa, mapazia yatakapoondolewa na ngozi kuchunwa, tutaona kile kilicho ndani ya ngozi. Kisha tutaelewa. Kwa hiyo, Kiyama ni *Zahur* (Siku ya Ufufuo, uwazi na udhihirisho). Vingenevyo, tungepata malipo yetu au adhabu katika ulimwengu huu wenyewe, kabla ya kifo. Athari ya dini ingelikuwa wazi hapa katika ulimwengu wenyewe.

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 35



Wakati tukienda kutoka upande huu mpaka kwenda kwenye upande mwingine, kila kitu kitakuwa wazi. Qur'ani inasema:

﴿ وَإِذَا ٱلْوُحُوشُ حُشِرَتْ ﴿٥﴾ ﴾

**Na wanyama pori watakapokusanywa**. (**Surah At-Takwir – 81:5)**

Siku ya Hukumu itakuwa kwa ajili wanadamu, sio kwa ajili ya wanyama. Hakuna dini kwa ajili ya wanyama. Hivyo ni nani hawa ambao wanatajwa kama wanyama katika aya hii? Kama vile ambavyo hakutakuwa na kuulizwa na Hukumu kwa ajili ya wanyama, hakutakuwa na Hukumu kwa watu walionunuliwa kutoka majangwani pia. Wanyama hawatakuwa wale (wanyama halisi) ambao wamenunuliwa kutoka majangwani, bali wale wanadamu ambao wamejigeuza wenyewe kuwa wanyama. Wakati ngozi zao zitakapochunwa, wanyama kutoka ndani yao watatoka nje. Kisha Malaika wataambiwa kuyaswaga makundi haya ya wanyama kwenda kwenye Jahannam.

Kwa hiyo, dini ni hitajio la kwanza la mwanadamu. Hewa na maji ni vitu muhimu sana kwa ajili ya mwanadamu; hawawezi kuishi bila ya hewa na maji. Tunadai serikali kutengeza barabara, kusambaza maji kuondoa uchafuzi. Kwa nini tunadai vitu hivi? Kwa sababu ni jukumu la serikali nzuri kufanya maandalizi kwa ajili ya mahitaji haya. Kama serikali inaandaa kwa ajili ya maji safi, chakula kizuri na mazingira safi na kutupatia mahitaji mengine muhimu, ni wajibu wake vilevile kutekeleza jukumu lake la muhimu zaidi; kutupa nafasi ya kuwa wanadamu wazuri na kwa madhumuni hayo huweka utekelezaji wa dini. Katika utawala wa Mtume (saw) hii ilikuwa ni hatua ya kwanza. Katika utawala wa Imamu Ali (as) hii ilikuwa ni hatua ya kwanza.

Kama mtu akielewa filosofia ya dini, basi vilevile hufahamu kile anachotakiwa kufanya kwanza. Aina gani ya uhusiano anapaswa kuuweka na dini? Sio sahihi kuchukua mkeka wa kuswalia, kukaa msikitini na kuji-

fikiria wewe mwenyewe kama mtu wa dini zaidi. Mtu bora zaidi ni yule ambaye hutekeleza dini kwanza kabla ya kukanyanga juu ya mswala. Haki hii walipewa Watukufu Maasumin (as) kutekeleza dini, lakini bahati mbaya hawakuweza kuwa watawala. Kwa nini? Ili watu wasijue kwamba dini ni haja ya msingi? Kama ilivyo leo sio watawala. Leo haja ya dini iko kwenye akili za watu lakini haiwezekani kuonekana kwenye maisha yao. Wanafikiria kuhusu dini. Haja ni kufanya mazingira ya dini na dini kutekelezwa na watu kwa sheria, ili kwamba mwanadamu apate nafasi ya kuwa binadamu.

## Swali

**Swali la kwanza:** Umesema kwamba dini sio kuhusu kuingia Peponi - (*Jannah*) na kwamba ni kwa ajili tu ya kukutana na Allah (s). naomba tafadhali uelezee hilo kwa urefu kwa sababu suala hili linahitaji kuelezewa kwa uwazi sana. Pili, umesema kwamba mwili wetu ni fremu na fremu hii inatakiwa kujazwa vitu fulani. Ni vitu gani hivyo? Tuishi vipi katika ulimwengu huu ili tuweze kujitengeneza wenyewe kuwa binadamu kamili na kufuata dini sawasawa? Kitu kingine ulichosema kilikuwa kwamba kuna watu wengi wenye elimu na wasomi ambao hawana dini na wanapata elimu kidogo ili kutusumbua. Ni jukumu gani linapaswa kuwa kwa wasomi wa kidini ili kwamba kizazi kipya hususan vijana waweze kujifundisha kuhusu dini?

**Jibu:** Nilikuambia kwamba dini sio tu kwa ajili ya kupata *Thawaab* (malipo), dini lazima ifuatwe kwa ajili ya Allah (s), haya ndio madhumuni yetu pekee.

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡإِنسَٰنُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدۡحٗا فَمُلَٰقِيهِ ﴾

**Ewe mwanadamu! Hakika wewe ni mwenye kufanya bidii kwa Mola wako, basi utamkuta. (Surah Al-Inshiqaaq -84:6)**

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 37



﴿ ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَـٰبَتۡهُم مُّصِيبَةٞ قَالُوٓاْ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيۡهِ رَٰجِعُونَ ١٥٦ ﴾

**Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake Yeye tutarejea. (Surah Baqarah -2:156)**

Maisha yako wewe sio kama maisha ya viumbe wengine ambayo ni kama mto ambao huanzia upande mmoja na kuishia upande mwingine. Mto katika hali nyingi huanzia milimani kisha huishia kwa kukutana katika bahari. Lakini mto wa ubinadamu sio kama mto ambao huanzia mlimani na kuishia baharini.Unaanzia kwa Allah (s) na kuishia kwa Allah (s). Wakati mwingine tunafikiri kwamba wakati tunapaswa kurudi kwa Allah (s), kwanza kwa nini tulileletwa, kwa nini safari hii ni muhimu; je safari hii ilikuwa lazima? Je, kulikuwa na njia nyingine, njia ambayo kwamba tulikuja nayo hatutarudia katika njia hiyo hiyo. Tulikuwa sio wakamilifu tulipojuja hapa, lakini hatutakwenda namna hiyo, tulikuwa kitu tofauti wakati tulipokuja na tutakuwa tofauti wakati tutakapokwenda.

Allama Iqbal ameilezea hii katika shairi lake "*katra aur darya*" (tone na bahari), kwa mfano, jinsi mawingu yanavyotengenezwa. Jua linawaka juu ya bahari kubwa, kwa ajili ya joto lake maji ya bahari huvukiza na kuwa mvuke ambao huenda kwenye angahewa na kuchanganyika na hewa na kisha huenda juu zaidi. Angahewa ya juu ni baridi kuliko ya chini; katika angahewa mvuke huwa baridi na kugeuka kuwa matone. Matone hujikusanya sehemu fulani na kuyageuza kuwa mawingu na kuwa mazito, na huja kwenye hatua ya chini ya angahewa, kisha upepo huyachukua kuyapeleka kwenye milima ambako hugongana na mlima na mvua hunyesha kutoka mlimani kwenda kwenye michirizi ya mito iliyo tupu, mwishowe hufika baharini tena. Ni yaleyale matone ya maji ya chimvichumvi kutoka baharini ambayo yamekuja kwenye mto kutoka milimani na kuwa baridi (yasiyo na chumvi), maji hayohayo ya chumvi yanaweza kuwa sababu ya kifo chetu kama tungekunywa hata tone moja kutokana nayo. Haya ni maji yaleyale ambayo kwamba kwa hayo tunaishi

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 38



leo; nani aliyefanya haya maji ya chumvi? Hubadilika kwa sababu ya safari yake. Yamepita kutoka kwenye joto na baridi, kutoka kwenye milima mpaka kwenye uwanda, mito na mifereji, hupita kwenye ardhi na kisha hutoka katika safari hii na kubadilisha ladha yake. Vitu vingi vimechanganyikana humo; madini yenye manufaa huchanganyika humo: maji ya bahari hayana vitu vyote hivi ndani yake, hivi hujichanganya ndani yake wakati wa safari yake. Mwishowe maji haya lazima hachanganyikane na maji ya bahari lakini baada ya safari ndefu. Mfano huohuo unaweza kuchukuliwa kwa wanadamu pia.

﴿ ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَٰبَتۡهُم مُّصِيبَةٞ قَالُوٓاْ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيۡهِ رَٰجِعُونَ ١٥٦ ﴾

**Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake Yeye tutarejea. (Surah Baqarah -2:156)**

Aya hii tunaisoma tunapopata habari za kifo chochote, hii ni kwa ajili ya watu walio hai tu ni kwa ajili yao tu, sio kwa ajili ya wafu, kila chembechembe ya ulimwengu husema sisi ni wa Allah tu na marejeo ni Kwake, kila chembechembe imekuja ikiwa pungufu na kurudi baada ya kukamilika. Ni kwa ajili ya ukamilifu wa mwanadamu kwamba chembechembe nyingine za ulimwengu hufanya safari yao kwa kutenzwa nguvu, wakati ambapo mwanadamu hufanya kwa hiyari (huchukuwa hatua zake mwenyewe, ambazo ni utashi wake).

Kwa mfano unasafiri kwa ndege au gari moshi na mtu mwingine anaimaliza safari hiyo kwa miguu, mtu huyo ni bora kuliko wewe, kwamba mwanadamu ni bora kuliko viumbe wengine, muonekano utakuwa kama uwezo wa mwanadamu utakavyokuwa, kwa mfano unaweza kukipa sura yoyote kinyunya cha unga wa ngano. Unaweza kutengeneza kutokana nao mkate, unaweza kuufanya wa mraba au wa mviringo kwa ulaini wake unaweza ukatengeneza kwa umbo lolote, uhalisia wa mwanadamu sio mwili wake au sio ndani ya mwili wake wala nje yake, kwa hakika mwanadamu ni jina la (roho) ambaye tunampa jina kama nafsi au mimi au

miye. Hiyo ni nafsi yetu lakini tumepoteza anwani yetu. Baada ya kukutana, kama mtu anamuuliza mtu mwingine ni wapi nyumbani kwake yeye mwenyewe? Utapatwa na mshangao juu ya swali hili kwamba hajui anwani ya nyumba yake mwenyewe; huenda amepoteza kumbukumbu yake, amesahau anwani ya nyumbani kwake mwenyewe! Yeye ni mkazi wa eneo hili, alizaliwa hapa, huenda kilichotokea kwake kinaweza kuwa ni kwa sababu ya joto kali amepatwa na mchanganyiko wa akili na amesahau anwani yake mwenyewe. Tunaandaa daktari au tunampeleka hospitslini. Hii ni kwa sababu ni kitu kisicho cha kawaida kwa mtu kusahau anwani yake mwenyewe.

Kama ukimuuliza mtu baada ya kuweka mkono wake juu ya mwili wako atasema huyu ni mimi mwenyewe, ni kama vile ukiweka mkono wako juu ya meza na kusema hii ni mimi, ni kosa kabisa huwezi kuwa meza, meza inaweza kuwa yako, lakini huwezi kuwa meza. Kwanza kabisa watu lazima watafute anwani yao, mtu ambaye ana fahari sana, nini ambacho anajifikiria yeye mwenyewe. Hakuna mtu anayejifikiria yeye mwenyewe kuwa duni kuliko mfalme wa wafalme au pengine waziri wa kawaida wa baraza lake la mawaziri, kila mtu ni mfalme wa wafalme ndani ya ulimwengu wake mwenyewe lakini hajui, amesahau "Umimi" (ubinafsi) wake, anwani yake, namba yake ya simu, anwani yake kamili, amesahau kila kitu, tumejipoteza wenyewe, watu wamepoteza watu, umimi umepotea kutoka kwenye mkono wake mwenyewe. Allah hukutana wakati watu wakijiona wenyewe.

مَنْ عَرَفَ نَفْسَهُ فقدْ عَرَفَ رَبَّهُ

**Kama unataka kumjua Mola wako, jijue wewe mwenyewe.**
**Imam Ali(a.s), *Gharrar Al Hikam***

Yeyote yule anayejigundua mwenyewe, humgundua Mola wake, yeyote yule anayejipoteza mwenyewe anampoteza Allah. Hiki ni kitendo cha mkataba kati ya nafsi na Allah; njia ya karibu sana ya kumfikia Allah ni

kupitia mtu yeye mwenyewe. Kwanza jigundue wewe mwenyewe, kisha utamfikia Mola wako, utamgundua Allah. Usiwe kama mtu ambaye anakuja kutoka nje anaweka mkono wake juu bega lako na kusema huyu ni mimi. Wakati mwingine tunakusanyika mahali fulani, ambako kama tunazungumza kuhusu siasa kila mtu anataka kuonesha kwamba hakuna mwanasiasa mkubwa kama yeye. Wakati tukizungumza kuhusu dini, mtu ambaye hakujifunza dini hata kwa siku moja na hajui chochote kuhusu dini au sheria zake, wakati wote atatoa maoni, atatoa *fatwa* (hukumu ya kidini) na kwa uhuru anatoa maoni yake kuhusu viongozi wa kidini wa Kiislamu, wahubiri na wanachuoni. Ni kama mtu ambaye amesahau njia ya nyumbani kwake mwenyewe lakini anawaelekeza watu wengine.

Vipi utamuamini mtu kama huyu? Iwapo sisi tu mwili, naulezea katika maneno rahisi sana, maneno mawili ni ya kawaida sana, moja wapo ni "mimi" na lingine ni "yangu". Tunayatumia maneno haya ambako kuna vitu viwili, kwa mfano nasema kitambaa (cha mkono) hiki ni changu, maana yake hapa kuna vitu viwili, moja ni kitambaa na cha pili ni mimi mwenyewe, moja ni mmiliki wa kitambaa, hapa mimi ni mmiliki wa kitambaa ndio maana ni changu, hatuwezi kusema changu kwa mimi, shati hili ni langu, kama nikisema mimi ni shati hili, utasema ni makosa. Mimi sio shati, lakini shati ni langu. Kama mimi ni kilemba hiki au kilemba hiki ni changu! Sasa nauliza kuhusu mkono wangu, iwapo mimi ni mkono au mkono ni wangu? Jibu litakuwa ni hapana. Mkono ni wangu, sasa nauliza kitu kama hicho kuhusu mwili wangu wote. Mimi sio mwili, mwili ni wangu. Sasa mtafute, ni nani mmiliki wa rasilimali hizi? Wakati nikizikwa, sio mimi, ni mwili wangu. Niko juu ya ardhi na kamwe sitaingia ndani yake. Ukweli wa ubinadamu sio mwili, kama nguo hii ambayo imeshonwa na fundi cherehani, itumie, wakati ikichakaa shona nyingine.
Katika hali hiyo hiyo, Allah aliumba mwili huu kwa ajili yangu na "Mimi" huyo ananufaika kutokana na nguo hii ambayo ni mwili. Kila wakati anapohitaji mwili, lazima aupatie nguo mpya. Imesemwa kwamba dini ni kile kitu ambacho humbadilisha mtu kuwa mwanadamu. Hivyo unahitaji tu kuelewa ni nini ukweli wa mwanadamu? Mwanadamu sio mwili tu, sio

umbo. Moja ya masharti ya dini ni kwamba mwanadamu lazima aamini katika yasiyo onekena (*Ghaib*). Mwana dini mchamungu ni yule ambaye huamini katika yasiyoonekena. Lakini chochote kilichoko nyuma ya kuta sio kisichoonekena (*Gharib*). Tunaona baadhi ya watu huzungumzia kuhusu yasiyoonekena, lakini kweli wanazungumzia kuhusu yasiyoonekana? Iwapo wanazungumzia kuhusu vitu vile ambavyo vimejificha nyuma ya kuta! Hivi sio visivyoonekena (*Ghaib*), hivi vimejificha! *Ghaibat* (kutokuonekena) ni kinyume cha *Shahadat* (ushahidi), *Shahadat* maana yake kuwepo kimwili au kiumbo, *Ghaibat* ni bila umbo au mwili. Haina umbo lolote, nafsi yako haina umbo.

Kama pikipiki yako ilivyo na mwili, wewe pia una mwili, nguo zako zina umbo pamoja na mwili. Hata mwili wako ni mwili vilevile lakini wewe mwenyewe sio mwili. Ukweli wa mwanadamu hauko hivyo, ni nafsi. Kwa hakika dini ni ile maada ambayo hufanya umbo la mwanadamu baada ya kukutana na nafsi. Hiyo inakuwa ya kiroho; dini ni jina la maada. Ina sehemu tatu; moja hutokana na elimu na pili na kitendo, elimu na kitendo vyote huwa maada na baada ya kukutana na nafsi inakuwa nafsi ya mwanadamu. Nafsi hii haiwezi kuchukua umbo lolote, kama ilivyo kwa unyunya wa unga, sasa umbo lolote utakalotoa kwenye nafsi hii italipata umbo hilo, sio tu ngozi bali vilevile kuna nafsi chini ya ngozi, katika Siku ya Hukumu wakati ngozi itakapoondolewa umbo halisi la nafsi litatokea. Kutakuwepo na maumbo mbalimbali ya nafsi; baadhi yatakuwa wanyama pori, ng'ombe wenye njaa, na huenda wanadmu wazuri pia. Kitu chochote kile ambacho kimechanganyikana na nafsi, kitachukua sifa kutokana nayo; kuna tofauti kubwa kati ya mtu wa dini na yule asiye wa dini, Allah anasema:

﴿ فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُۥ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُۥ ﴿٨﴾ ﴾

**Basi anayetenda wema sawa na chembe atauona! Na anayetenda uovu sawa na chembe atauona! (Surah Al Zalzala; 99:7-8)**

Chukulia kama unachora picha na wakati huohuo nadhari yako imegeuzwa na kitu fulani, kwa mfano Tv, lakini uchoraji wako unaendelea, ni umbo gani litajitokeza? Kalamu iko mkononi mwako na hivyo itaandika cho-

chote utakacho iwapo ni sahihi au kosa. Kama mtu anachora msitari baada ya kuushikilia mkono wako; msitari utachorwa amma wa kunyooka au wa kupinda! Kama mwashi ataweka vifaa vyake (dongo ulaya, mchanga nk.) hapa na pale juu ya ukuta, bila ya shaka atakuwa hakupoteza vifaa vile, lakini umbo la ukuta ule litakuaje?

Hizi ni hatua za uzalishaji wako, unajfanya mwenyewe kwamba ulikuwa hujakamilika pale wakati ulipokuja hapa. Unakuwa ni mtu unayejitengeneza mwenyewe, unatengeneza jengo la uwepo wako, na Allah (s) amekupa elimu. Sehemu ya pili ya nafsi ni kufuata kitendo baada ya ukamilishaji wa mchakato wa jengo hili. Ngozi itaondolewa na mwanadamu wa kweli atatokeza nje. Sasa usiseme chochote kile ambacho umepata kukisikia, ni kiasi hicho tu ndio kilichoko akilini mwetu, unaamua kwamba hujui chchote kuhusu dini na nchi yetu kwa vile wewe sio Alexander, mshindi wa ulimwengu, lakini je, sisi wote hatujifikirii wenyewe kama Alexander? Hakuna mtu ambaye ni Elixander hapa, kwa vile serikali yetu ni ya kibepari na katika aina hii ya serikali kila mtu ni mwinyi. Hata akiwa nacho au la, hata kama hana pesa kwa ajili kuvuta (tumbaku) pia mtindo wake wa kutembea na kuongea ni kama wa kimwinyi; hata omba omba anayemuita omba omba mwingine, huzungumza katika mtindo wa kimwinyi. Kila mwanajamii wa jamii maisha yake huishi katika mtindo wa kimwinyi, wanashughulika na wake zao katika mtindo uleule wa kimwinyi, wanaongea na watoto wao na marafiki zao katika mtindo huohuo. Kama wakipata kazi fulani serikalini wanawaona wengine kama watumishi, wale ambao hupata kazi katika idara ya polisi huwafanya wengine kama watumwa, kamwe hawesemi kaa pembeni, siku zote husema ninakuja, ondoka njiani. Katika nchi yetu imekuwa ndio hali halisi, mwinyi kamwe hatoi njia bali watu wa kawaida huhitaji kutoa njia, kamwe hatufikiri kwamba picha ya dini ambayo ilijengwa katika akili zetu sio dini sahihi, lazima tuibomoe nyumba hii ya kinyamkera.

Ili kuifuata dini itatupasa tuibomoe nyumba hiyo. Wakati ukijenga nyumba nzuri lazima ubomoe miundo ya zamani na iliyovunjika. Bila ya kuibo-

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 43



moa, huwezi kujenga jengo jipya, kama unataka kufanya jengo imara badala ya nyumba ya muda bila kuvunja nyumba ya muda huwezi kujenga nyumba ya kudumu. Lakini kama mtu akisema nyuma zote (ya zamani na mpya) lazima zibakie katika sehemu hiyohiyo, haiwezekani. Hivyo kama unataka kujenga nyumba nzuri lazima ubomoe nyumba ya zamani, na kutupa kifusi chake mbali na eneo ambako huwezi kukiona kifusi hicho tena. Vilevile dini iko kama hivyo, chochote ambacho tumekiweka katika akili yetu lazima kiondolewe; bila ya kukiondoa itakuwa kama banda na nyumba nzuri sehemu moja, hakutakuwa na nyumba wala banda na vyote vitaharibika.

Kwanza lazima tuamue kwamba hatujui dini. Tumesikia mengi na kwetu sisi kila tulichosikia hicho ni dini. Ushuhuda wetu wote wa dini umetegemea katika kuwasikiliza wahutubu (Masheikh). Hatuna uwezo wa kunukuu rejea kutoka kwenye Qur'ani na Hadithi. Chanzo chetu pekee cha kupata (mafundisho ya) dini siku zote kimemekuwa ni masikio yetu. Na kama Mitume wangelijua chanzo hiki, wangekijumuisha hiki katika mafundisho yao na wangetuambia tujifundishe Dini kutoka kwenye Qur'ani, Hadithi na masikio yenu!

Hii sio hatua ya kwanza lakini mtu ambaye anachukuwa hatua hii ya kwanza, hatua ifuatayo itakuwa rahisi kwake. Tunafanya sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi na kuwaalika watu mashuhuri katika kuitekeleza sherehe hiyo mbele yake. Bila ya msingi hatuwezi kusimamisha jengo kubwa kama hilo. Jiwe la msingi maana yake ni jiwe la kwanza la Dini, ile nyumba ya mwanaserere ambayo ilijengwa mapema, nyumba ya kuwazika na fikira binafsi lazima ibomolewe. Kinachokusudiwa hapa ni kwamba tumekuwa tukifundishwa dini kuanzia utoto wetu kupitia wahenga na wazazi wetu. Hatukujifunza dini. Kama tunataka kujifundisha, basi kwanza lazima tuvunye kasumba hii akilini kwamba dini ya wazee wetu ni sahihi. Lazima tutambue makosa yetu na kisha ndio hapo tu tunaweza kuyasahihisha.
Tuna chanzo kimoja tu cha kujifundisha dini ambacho ni kufuata dini ya wazee wetu wakati ambapo kwa mujibu wa wanachuo (Maulamaa) kuna

vyanzo mbalimbali, Sharia (*fiqh*), Qur'ani, *Sunnah*, *Ijma* (kongomano la wanachuoni), *Aqil* (akili). Lakini katika bara letu (India-Pakistan) kuna chanzo kimoja tu na hicho ni kusikiliza (maana yake tunajifunza dini kwa kusikiliza tu)[1] kwa sababu ya hilo kamwe hatutoi nukuu ya Qur'ani, Hadithi, *Ijma* au *Aqil.* Siku zote tunasema tumesikia kama hivyo, tumeambiwa hivyo, hatujasikia kama hivyo, nk.

Chochote ambacho tumekipata kwa kusikia tu, hiyo sio dini ya kweli. Kwa kujifunza na kuilewa Qur'an na *Itrat* (mafundisho ya Ahlul Bayt (as)), chochote tunachokipata ni dini halisi, kwa kufuata dini hii muundo wowote tunaofanya huo utakuwa ni ubinadamu. Na hiyo ni hatua ya kwanza, msingi ambao ni vigumu kuuweka katika sehemu yake.

Kwanza weka msingi wako wa dini na kisha anza kujenga juu yake. Karibisha rafiki zako na waambie kwamba umebomoa nyumba ya zamani na kutupa mbali kifusi chake, waambie waje na lawalawa kwa sababu ni siku ya msingi wa ubinadamu na dini. Mpaka tutakapochukua hatua hii, hatuwezi kufikia kiwango hicho cha ukamilifu – Hali ya Ubinadamu kamilifu. Tunaendelea kuishi katika mabanda yetu ya zamani; na kama tunaendelea kuishi katika mbanda yetu ya zamani, yataendelea kujinyonya yenyewe na sisi pia na kisha siku moja yatatuangukia.

**Swali la pili:** Ni matokeo gani ya kutoifahamu Filosofia ya dini? Hata kama tunashiriki dini kwa ajili ya faida kuna tofauti gani?

**Jibu:** Moja ya vipimo vya kasoro zilizotengenezwa katika dini ambayo yenyewe ni kipimo kikubwa ni kwamba Filosofia ya dini, madhumuni na lengo la dini limefisidiwa kwa vivutio ambavyo vimo ndani ya dini. Ufisadi wa nadhumuni pamoja na faida na vivutio vimekuwa na nguvu juu yetu wote. Vivutio na faida vimekuwa madhumuni na madhumuni

[1] Hali ni hiyohiyo hata katika bara la Afrika. Tunajifunza dini kwa kusikiliza mihadhara na hutuba za Masheikh wetu. (Mtarjuma).

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 45



yamegeuka kuwa faida. Madhumuni ni vitu vile ambavyo kwamba kwavyo Allah (s) ameumbia dini, wakati ambapo faida na vivutio ni vitu vile ambavyo ni njia kwa ajili ya kuwageuza watu kuelekea kwenye dini. Kwa mfano elimu ina madhumuni na kuna vivutio fulani kwenye dini. Sasa chochote kitakachokuwa ni madhumuni ya elimu lakini katika nchi yetu madhumuni ya elimu ni kupata ajira. Haya ndio madhumuni ambayo tumeyaweka kwa ajili ya dini, yaani kupata kazi nzuri. Hili ni tusi kwa elimu na ni mkengeuko katika elimu. Kama ilivyotajwa awali jografia ya dini na kila kitu kimevurugwa.

Sasa hebu tuchukulie kwa wakati huu kwamba haya ni madhumuni ya elimu lakini hata katika hali hii mtoto haonyeshi kuvutiwa kwenye elimu; ni wazazi ndio ambao wanajali kuhusu elimu yake. Ili kumfanya mtoto avutiwe na elimu wazazi na walimu hutoa ahadi nyingi ya wanaserere, baiskeli, siku za mapumziko nk. ili kwamba mtoto kwa ajili ya kupata manufaa hayo ahudhurie shule na kuzingatia elimu. Wakati mtoto huyohuyo anapokua kidogo, mizani ya ahadi vilevile huongezeka, kwa mfano sasa anaahidiwa kupewa pikipiki au gari kama akimaliza masomo yake. Vivutio vyote hivi ni kwa ajili ya elimu, lakini ni nini madhumuni ya elimu? Madhumuni halisi ya elimu ni kumtengeneza mwanadamu mwenye heshima, mwenye elimu aliye hitimu, wakati ambapo katika nchi yetu madhumuni ni kupata kazi. Mtoto mdogo huhudhuria shule na kusoma kwa ajili ya kupata vitu alivyoameahidiwa kama pikipiki, gari, lawalawa, mandari nk. wakati ambapo upataji wa vitu hivi sio madhumuni ya elimu. Ni kutokomaa kwa mtoto ndiko kunakomfanya afikirie manufaa haya kama lengo na madhumuni, na hufanya juhudi kubwa katika elimu kwa ajili tu ya kupata vitu hivi. Lakini wale ambao wana utambuzi wa madhumuni hawahitaji vitu vya kuvutia na ahadi hizi.

Allah (s) aliumba dini kwa malengo na sambamba na madhumuni pia aliumba vivutio na manufaa ili kwamba wale ambao hawajakomaa na hawana utambuzi sahihi wa madhumuni ya dini, bado wanaweza kuja kwenye dini kwa ajili ya manufaa. Lakini kuna wanadamu kama hawa pia ambao huse-

ma kwamba: “Ee Allah! Ali hakuabudu Wewe kwa ajili ya tamaa ya pepo au kwa hofu ya Jahannam, Ali anakuabudu kwa sababu ya kwamba unastahiki kuabudiwa.”

Madhumuni ya dini ni kumchukua mtu kwenye vilele vya juu vya ubinadamu. Leo ulimwengu wote unapita kwenye migogoro mbalimbali; migogoro ya kiuchumi, migogoro ya kisiasa, migogoro ya kiusalama. Lakini migogoro yote hii imetengenezwa na watu na ni ya muda; sio yenye madhara sana ambayo inaweza kuwafanya wanadamu wote wawe katika wasiwasi. Mgogoro ambao lazima ushitue na kumfanya kila mtu kuwa na wasiwasi ni mgogoro unaoendelea hivi sasa katika nchi za Mashariki na Magharibi, kwa Waislamu na wasio Waislamu; mgogoro wa ubinadamu; mwanadamu haonekani popote. Allama Iqbal ametafsiri fumbo hili kutoka kwa Maulana Rum kwamba siku moja mtu mwenye busara sana na akili alikuwa akihangaika akizunguka katika mji akiwa na taa mkononi mwake. Watu wakamuuliza alichokuwa anatafuta. Akajibu kwamba namtafuta mwanadamu. Watu wakamuuliza: je, huwezi kumuona? Akasema nimejaribu kutafuta sana lakini sikuweza kumpata hata mmoja. Huyo ninayemtaka sikuweza kumpata.

دی شیخ با چراغ نمی گشت گردِ شہر
از دِیو و دد ملولم و انسانم آرزوست

Sheikh mmoja wakati wa mchana, alikuwa akitafuta kitu fulani akiwa na taa mkononi mwake. Wakati alipoulizwa: vipi? Alisema nimechoshwa na wanyama na hivyo namtafuta mwanadamu.

کفتیم کی می پیدا نہ شود گشتہ این ما
گفتا کہ این پیدا نہ شود ہم آنم آرزوست

Alipoulizwa, unatafuta kwa bidii sana, bado huwezi kuona mwanadamu? Akajibu, ndio yule ninayejaribu kumtafuta bado hajaweza kupatikana.

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 47



Ni lini hilo litaweza kupatikana? Wakati likifanywa tu, basi hapo ndipo linaweza kupatikana. Dini imekusudiwa kujenga na kumtengeneza mwanadamu. Ni dini ambayo humpa mtu ilani ya ubinadamu. Kipimo kijenzi cha dini hujulikana kama "*Akhlaq*" (maadili); utengenezaji wa hulka - *Khulq*; kama ilivyotajwa kabla *Khalq* ilitengenezwa na Allah (s), lakini *Khulq* lazima ijengwe na mtu mwenyewe. Mulla Sadra mwanachuoni rasilimali wa Shia, ambaye kwamba kwake yeye inaweza kusemwa kwa kujiamini kwamba baada ya maasumin (as) na masahaba wao wa karibu hakuna aliye mashuhuri kama yeye ambaye ni mwanafalsafa wa Kiislamu anayeongoza. Yeye anasema: "Ewe mwanadamu! Umbile lako la kimwili (*Khalq*) limefanywa na Allah na sasa lazima ujenge khulka *(Khulq)* yako. Jinsi Allah (s) alivyoumba kwa uzuri *Khalq* yako, hivyo sasa wewe pia lazima uijenge Khulq yako kwa uzuri kiasi hicho hicho. Mwanadamu wa kweli ni jina la *Khulq* bora ndani ya kiumbe hiki bora (*Khalq*)."

Kwa hiyo hatupaswi kupoteza umbile letu hili zuri kwa kutokuendeleza Khulq hii nzuri ndani yake. Haya yalikuwa madhumuni na mwenendo wa Maasumini (as), yaani kujenga Khulq bora ndani ya kiumbe bora vinginevyo mwanadamu ataangamia. Kuna tofauti kati ya mtu mwenye ngozi nzuri na mwanadamu ndani ya ngozi; vazi maridadi na mtu bora ndani yake. Allah ameumba muonekano wa nje wa mtu kwa uzuri na akamuambia mtu kufanya muonekano wake wa ndani kuwa mzuri. Ngozi ya mtu na nje yake ni nzuri lakini vipi kama ubinadamu uliopo ndani yake sio mzuri? Kama Khulq haipo, basi mtu huyu mbele za Allah (s) sio bora; ni kama mnyama mzuri tu. Uzuri ni sifa ya kila kitu. Miti, mimea na wanyama pia ni wazuri kama Allah (s) alivyosema katika Qur'ani kwamba tumeumba hiki kijani, hii miti kwa ajili ya kuipendezesha ardhi. Tunapanda miti ndani ya nyumba zetu na kufikiria kwamba tumekuwa wenye kupendeza. Haijalishi ni miti mingapi umepanda, mitungi mingapi ya maua uliyoweka na bustani mbalimbali ulizotengeneza ndani ya nyumba yako, vyote hivi vitaifanya ardhi kuwa ya kupendeza lakini sio mtu. Manukato ya maua yataifanya hewa kuwa nzuri lakini sio mtu yule anaye-

vuta hewa hii. Haijalishi ni kiasi gani cha manukato unaweka katika mwili wako, itafanya tu ngozi yako kunukia vizuri lakini sio mtu ndani yake, haijalishi ni kiasi gani cha krimu unachoweka, itafanya tu ngozi yako kupendeza lakini sio mtu ndani yake. Basi kipi kinamfanya mtu kuwa wa kupendeza? Ni *Khulq* ndio humfanya mtu kupendeza. Rangi hufanya kuta kupendeza lakini sio mtu; kwa kuvaa nguo nzuri ni kupendeza kwa nguo ambako hudhihirika lakini bado mtu hachukuliwi kama aliyependeza.

Mfano wa hoja hii ambao huenda umeusikia ni ni kuhusu urembo wa Nabii Yusufu (as). Tunafikiri na tuliambiwa uzuri wa Nabii Yusf (as) ulikuwa katika ngozi, kidevu na mashavu yake, paji lake la uso, nywele zake, na midomo yake. Sio kwamba vyote hivi vilikuwa havipendezi, lakini hebu itazame Qur'ani ili uone ni uzuri gani wa Yusuf unaotajwa na Qur'ani. Lazima usome Qur'ani mara kwa mara mpaka wakati Qur'ani itakapoonyesha siri ya urembo wa Nabii Yusuf (as). Qur'ani haifichui siri zake kwa watu wasio na ujuzi (*Na Mahram*), hivyo lazima kwanza uwe na ujuzi wa Qur'ani kwa kiasi kwamba Qur'ani inaanza kuzungumza na wewe na kufichua siri zake kwako.

Kwa kawaida ni ukweli unaokubaliwa kwamba mwanaume anapendeza zaidi katika ujana wake ukilinganisha na wakati ndevu na masharubu zinapoota kwenye uso wake. Hii ndio sababu kwamba watu hunyoa ndevu na masharubu yao ili waonekana wamependeza. Lakini tena huku ni kutokuelewa kwamba kwa mtu kunyoa nywele atapendeza, kama ni hivyo basi wale wanaopoteza nywele zao za kichwa kwa nini wanakuwa na wasiwasi? Hivyo kwa hakika kwa kunyoa nywele ndevu hutaonekana wa kupendeza.

Wakati mke wa Waziri aliposhindwa kumshawishi Yusuf na akashikwa alilaumiwa na akatetewa na wanawake wengine. Ili kuthibitisha uovu wake kwamba alikuwa hana hatia, alimkaribisha Yusuf na akawafanya wanawake wa familia za mamwinyi ambao walikuwa wakimsuta kwa msimamo wake huo wakiwa na visu na matufaha mikononi mwao. Alimleta

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 49



Yusuf kutokea mlangoni. Wakati wanawake hawa walipomuona Yusuf badala ya kukata matufaha kwa kisu walikata vidole vyao. Hapa lazima utafakari kwamba je, hii ni mara ya kwanza kwa Yusuf kuja mbela za watu na mbele za wanawake? Wakati Yusuf alipotolewa kisimani na msafara na kisha kuuzwa sokoni alikuwa kijana na mrembo zaidi kuliko sasa. Basi kwa nini hakuna mtu yeyote aliyekata mikono yao au kuuma midomo yao wakati huo. Wakati Yusuf alipokwenda kwenye baraza ya mfalme alikuwa amevaa joho zuri la kupendeza na mchangamfu kisha hakuna aliyekata mkono wake. Yusuf alikulia mbele ya mke wa waziri, na kuwa kijana mdogo, kisha kijana mkubwa ndevu na masharubu zikaota usoni mwake. Huu ndio wakati ambao mke wa waziri kapatwa na nia ya uovu kwa Yusuf na akajaribu kumshawishi kihila. Hivyo ili kuokoa uso wake na kuthibitisha kwamba ilikuwa ni kitu cha kawaida kwa mwanamke aliwakaribisha wanawake na kumfanya Yusufu apite kati yao. Swali linalokuja ni kwamba kama wanawake walizimia na kukata mikono yao kwa kuangalia uso wa Yusuf basi wangefanya hivi kabla wakati Yusuf alipoletwa kutoka sokoni. Wakati ule Yusuf alikuwa anapendeza zaidi kuliko leo wakati ana ndevu na mashurubu. Wangelikata mikono yao wakati ule wakati alipokuwa kijana mtanashati zaidi. Lazima tutafakari juu ya kile Qur'ani inachosema hapa. Inasema kwamba wale wanawake ambao walikata mikono yao walikuwa hawaangalii uso wa Yusuf, mshangao huu ulitokea wakati walipoona mwenendo na tabia ya Yusuf.

Walikuwa wanaangalia uso wa Yusuf kila siku lakini leo wametambua mwenendo wa Yusuf. Wakati waliposhuhudia mwenendo wa Yusuf hawakuweza kuamini kwamba kijana mtanashati kama huyo na fursa zote za kutenda dhambi ya starehe mbele yake; mwito wa uovu ulikuwa pale, hakuna mtu wa kumuona, mlango ulifungwa, mazingira ya utongozaji yalitengenezwa na katika mazingira haya yasiyoepukika, Yusuf akiwa na hofu ya Allah anasema kwamba "Tahadhari! Yusufu hawezi kusogelea uovu." Huu ni mwenendo ambao hutetemesha mikono ya kila kitu. Huu ndio uliokuwa urembo halisi wa Yusuf.

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 50



Urembo huu na hadhi haukuwa ule uliopo katika muonekano wa nje wa kiumbe; ilikuwa ni hadhi na urembo wa *Khulq*. Hii sio hadhi ambayo Yusuf alipata kwa kuzaliwa nayo badala yake huu ni urembo ambao Yusuf aliuendeleza ndani ya nafsi yake. Hadhi hii iliwafanya wanawake wazimie. Kisa hiki ndani ya Qur'ani ni kwa ajili yetu, kwa ajili ya vijana wetu kwamba hawapaswi tu kuwa wahafidhi wa Sura hizi za Qur'ani, bali lazima wapate ujuzi wa siri za Qur'ani. Vijana lazima wapate siri za umri wa ujana, siri za urembo na lazima waelewe chanzo halisi cha kupata urembo na hadhi ya kweli ya ubinadamu. Allah (s) amewafanya wahubiri wa urembo wa *Khulq* wale ambao wenyewe ni warembo katika uoni wao wa nje pia, Maimamu watukufu (as). Lakini wakati mwingine urembo huu wa kweli unachafuliwa na kupata harufu mbaya ndani yake. Kuna baadhi ya vitu ambavyo hung'arisha urembo wa mtu; vitu hivi ni maadili, mwenendo mzuri na tabia njema, lakini pia kuna vitu ambavyo huchafua urembo huu.

Idadi ya watu wenye tabia mbaya na sifa za uovu sio wale ambao wana sura mbaya. Leo ambaye anauchoma ulimwengu, sio wale ambao sura zao na mwili ni mweusi, ambao sura zao hazipendezi lakini ni kutoka kwa wale ambao wanajiona miili yao ni mizuri na ni weupe. Ni kwa sababu yao ubinadamu unaungua; ni kwa sababu yao kwamba ulimwengu wote wa Waislamu umefikia kwenye taya za kuangamiza.

Leo Pakistana imekuwa sio salama na kila mji wa Pakistan umekuwa ni nyumba ya machinjio kwa raia zake wenyewe; wanauawa na nani? Sio kwa sababu ya wale wanaolipwa ili kufanya mambo hayo. Allah (s) ametupa akili na lazima tuzitumie. Ni mfano mzuri sana kwamba wakati mbwa anatupiwa jiwe na kama mbwa huyo ni kichaa atauma lile jiwe, lakini kama sio kichaa humfukuza yule aliyemtupia jiwe. Kama akili hii Allah (s) amewapa wanyama basi mwanadamu anategemewa kuwa na akili zaidi na kuonesha ukakamavu zaidi wa akili. Kama leo mtu fulani anatuuwa sisi katika Pakistan hatupaswi kuanza kuuma mawe, lazima tuangalie ni nani yuko nyuma ya mauaji haya; nani aliyetupa mawe haya? Leo tunafurahi

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 51



tunaposikia habari kwamba operesheni fulani imeuwa magaidi fulani na kuwazingira katika eneo fulani. Lakini swali bado linabakia kwamba ni nani aliyeutengeneza ugaidi huu?

Hutokea katika vijiji ambako kuna mfumo wa kimwinyi. Mwinyi siku zote ana baadhi ya watu wakorofi aliowakodi, hivyo kama mtu akileta upinzani kwa mwinyi huwatuma wakorofi hawa usiku ili kuwapiga wapinzani wale. Wakati kipigo hiki kikubwa kikiendelea mwinyi huyu mwenyewe huwasili kwenye eneo lile kama mwenye huruma na kupiga kelele na kuwapiga mateke wakorofi wale. Kwa njia hii wapinzani hao sasa wanakuwa wanyenyekevu kwake na kumshukuru mwinyi yule kwa fadhila zake. Hapa ndipo tunatakiwa kuwa na akili na katika hali hii badala ya kumshukuru mwinyi yule lazima tumchape usoni na kumuambia kwamba wewe ndiye uliyewatuma wakorofi hawa kutupiga na sasa unawapiga ili kutuonesha kwamba unatufanyia sisi upendeleo. Halikadhalika wale ambao wanaendesha operesheni hizi dhidi ya magaidi hawapaswi kupata shukurani, lazima tuwaambie kwamba ninyi ni viumbe msio na aibu ambao mmewatengeneza magaidi hawa, na sasa wakati magaidi hawa wanasakama makoo yenu mnaendesha operesheni ili kuwaangamiza. Lazima tuwaambie kwamba damu ya watu wasio na hatia wa taifa letu, damu ya wenye kukandamizwa inapaka mapaja na mabega yenu.

Sasa majinai yote haya ambayo yanafanywa juu ya ardhi, yanatokea kupitia ngozi hizi nyeupe na hata kama wengine wanaosha mikono yao kwa hakika wako nyuma yao. Sio watu wazuri. Ngozi nyeupe sio urembo, basi uko wapi urembo? Kama unataka kuona basi njoo na uone ubora uliopo ndani ya Bilal. Rangi ya Bilal ilikuwa nyeusi lakini Bilal alipoadhini humpa amani na furaha Mjumbe wa Allah (saw). Kulikuwa na wasomaji wengi wazuri waliokuwepo wakati ule na wenye sauti nzuri sana, matamshi ya Kiarabu, wale ambao waliweza kutamka "*Shin*" kama "*Shin*" lakini mpaka wakati ule kama Bilal hajaadhini, Mjumbe wa Allah (saw) hatoki kwenda msikitini. Huu ni urembo ndani ya mtu huyu mwenye ngozi nyeusi na urembo huu umejengwa kutokana na Maadili, lakini kuna vitu

fulani ambavyo huchafua urembo huu pia.

Kwa hiyo kama filosofia ya dini haikueleweka na tunaikubali tu dini kwa ajili ya manufaa basi tutakwenda mbali sana na ujenzi wa *Khulq* ambayo maana yake ni ubinadamu. Kwa matekeo haya wote wanadamu wenye dini na wasio na dini wataonekana katika jamii, lakini bila maadili. Tutakuwa tumeona sisi wenyewe kwamba wako wachamungu wengi ambao hata hawakosi sala za sunna na hujaribu kufanya kila kitendo cha malipo (*Thawaab*), lakini wakati huohuo wana maadili mabaya sana na familia zao wenyewe, wanadanganya katika biashara na wanahusika na maumivu ya Waislamu wengine. Hivyo kujenga Khulq ndani ya mtu ni muhimu sana kwa maisha ya jamii ambayo haiwezi kufanywa bila uelewa na kupata ujuzi wa **Falsafa ya Dini.**

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 53



## Machapisho mengine

**The System of Wilayat in the vision of Qur'an**

**Philosophy of Qayam-e-Hussain**

**Values of Ashura**

**Tragedy of Qods**

**The Candle of the Path of Allah**

**Mashrabe Naab – Goods for Humanity**

**Defeated Velvet Revolution in Iran**

**Azadari – A movement by Lady Zainab (s.a)**

## Upcoming Publications

**Role Model and Character**

**An exposition of Ziarat-e-Ashura**

**The Role of Saudi Arabia in Muslim world**

**Pakistan Political Journal – O Ignorant think about your nation!**

**Hussain – The Inheritor of Prophets**

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 54



## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 55



27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 57



87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 58



114. Iduwa ya Kumayili.
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?

140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Kati ya Alama kuu za dini Swala ya Jamaa.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya Pili
161. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
162. Falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Huduma ya Afya katika Uislamu
164. Hukumu za Mgonjwa

165. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein
166. Uislamu Safi
167. Majlis ya Imam Husein
168. Mshumaa
169. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
170. Uislam wa Shia
171. Amali za Makka
172. Amali za Madina
173. Uislamu na mfumo wa Jamii ya dini nyingi
174. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
175. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
176. Elimu ya Tiba za Kiislam Matibabu ya Maimamu
177. Falsafa ya Dini

# BACK COVER

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 61



Kitabu hiki huelezea kwa ujumla falsafa na hekima ya dini na jinsi ya kuifuata dini pamoja na changamoto zake. Mwandishi ameandika kitabu hiki kwa kuwalenga Waislamu wa Pakistan na India ili kuwaasa kwa ajili ya masaibu wanayoyapata mikononi mwa mabeberu. Lakini hali hii ipo pia katika nchi nyingine za Kiislamu, kama vile Iraq, Afghanistan, Palestina, na inanyemelea nchi nyingine za Kiislamu na kwa Waislamu popote wanapoishi ulimwenguni. Hivyo, ni jukumu la kila Mwislamu popote alipo kuchukua tahadhari na kuungana na Waislamu wote ulimwenguni kuukataa unyanyasaji huu unaofanyiwa Waislamu.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**

**Alitrah Foundation**

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv-com

Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 62

Filosophia ya Dini check Lubumba.qxd 7/1/2011 3:32 PM Page 63